# BRELA

## WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA LESENI

ISSN: 000401 | Toleo No. 08 | Januari - Machi, 2024



# MIAKA MITATU YA SAMIA NA BRELA


BRELA
WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA LESENI
BRELA HOUSE
*152*00#
Chagua 9
Kisha 2
Pakua
eMrejesho
Mobile App
Ingia katika
Google play
Tafuta emalalamiko
Jengo la BRELA, Kitalu Na. 20, Kiwanja Na. 23
Sokoine Drive / Mtaa wa Shaaban Robert
S.L.P 9393, 11101, Dar es Salaam, simu: +255 22 2212800
Barua Pepe: ceo@brela.go.tz • usajili@brela.go.tz
Tovuti: www.brela.go.tz
Tovuti: www.brela.go.tz
brela_tanzania
BRELA Tanzania
brela_tanzania
+255 (0) 735 331 003
BRELA ONLINE TV

# YALIYOMO


3 MIAKA MITATU YA SAMIA:BRELA YACHANJA MBUGA KUIMARISHA HUDUMA



6 KIJAJI AZIAGIZA TAASISI ZINAZOTOA LESENI KUKAGUA VIWANDA VINAVYOZALISHA MABATI



7 BURUNDI, SUDAN KUSINI WAELIMISHWA KUHUSU UTOAJI HUDUMA KWA NJIA YA MTANDAO



8 KAMATI YA BUNGE YASIFU UTENDAJI KAZI WA BRELA




BRELA
BUSINESS REGISTRATIONS AND LICENSING AGENCY

# TAHARIRI



***Bw. Godfrey Nyaisa***
*Afisa Mtendaji Mkuu BRELA*

Kwa heshima kubwa, nawakaribisha kusoma Toleo letu la Nane la Jarida la Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA). Hili ni toleo maalum lililosheheni mkusanyiko wa habari mbalimbali zinazoakisi mafanikio ya utekelezaji wa majukumu ya Taasisi yetu katika miaka mitatu ya uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita ya mama yetu mpendwa, Mhe. Samia Suluhu Hassan.

Nafarijika kwamba Taasisi yetu iliuanza mwaka huu 2024 kwa matumaini makubwa ya kuendelea kujiimarisha ili kufikia lengo letu la kuwa kituo ya mfano kikanda katika utoaji wa huduma bora za sajili na leseni za biashara.

Hili limedhihirika kufuatia ziara ya wajumbe kutoka Jamhuri ya Burundi na Sudan Kusini waliokuja nchini kujifunza utoaji wa huduma kwa njia ya mtandao unaotekelezwa na BRELA.

Kama Taasisi, tumejipanga kuendelea kuimarisha mifumo ya kisheria na kitaasisi ili kuwezesha upatikanaji wa huduma za urasimishaji na uendeshaji biashara kwa urahisi.

Kwa kushirikiana na wadau wetu, tunafanya jitihada za makusudi za kuboresha utendaji wetu kwa kurekebisha Sheria tunazosimamia na kutekeleza ili kuwahudumia wafanyabiashara na kuhakikisha biashara zao zinakua kwa kuzingatia mabadiliko ya biashara.

Katika kuhakikisha wateja wengi na wadau wetu wanafikiwa wakati wowote na mahali popote walipo, tumekuwa tukitekeleza mkakati wa kutoa elimu ya upatikanaji wa huduma kupitia mfumo wa usajili kwa njia ya mtandao na jinsi Taasisi inavyotekeleza majukumu yake kwa ufanisi na weledi katika kujenga mazingira wezeshi kwa maendeleo ya biashara nchini.

Taasisi imekuwa mstari wa mbele kuwajengea uwezo watumishi wake ili kuongeza ufanisi, na hivyo kung'ara katika utoaji wa huduma zake. Mafunzo yametolewa kwa wadau mbalimbali wakiwemo wanafunzi, wanawake, vijana na wawekezaji kupitia warsha, semina pamoja na kushiriki kwenye maonesho mbalimbali.

BRELA inafanya jitihada za kuhamasisha na kutoa elimu kwa umma kwa kuandaa maudhui yanayotolewa kupitia televisheni, redio, magazeti, mitandao ya kijamii pamoja na jarida hili kwa ajili ya kuwapa elimu kuhusu mifumo ya sajili na leseni kwa njia ya mtandao, suala ambalo limepewa kipaumbele katika kuimarisha shughuli na huduma za Wakala.

Taasisi hii imejenga ukaribu na ushirikiano na wadau kwa kujiwekea utamaduni wa kutuma ujumbe kwao kuwakumbusha wajibu wao katika kuhuisha taarifa zao za kila mwaka na kuhuisha leseni za biashara na viwanda kupitia mtandao.

Kwa heshima na taadhima, nawatakia usomaji mwema wa jarida hili kwa kukaribisha maoni kuhusu namna ya kuliboresha ili kujenga uhusiano mzuri na jamii yetu na kufikia matarajio yenu.

"Kwa kushirikiana na wadau wetu, tunafanya jitihada za makusudi za kuboresha utendaji wetu

**BODI YA UHARIRI**

**Andrew Mkapa -** Mwenyekiti
**Theresa Chilambo -** Katibu

**WAJUMBE**

Meinrad Rweyemamu
Tawi Kilumile
Abdul-rahman Twaha Songoro
Neema Kitala
Yusuph Nakapala
Tulizo Mpina

# Miaka mitatu ya Samia: BRELA yachanja mbuga kuimairisha huduma

**Na Christina Njovu**

Salamu: "Jamhuri ya Muungano wa Tanzania: Witikio: Kazi Iendelee." Siku hizi salamu hii popote inapotamkwa, hakuna Mtanzania asiyeifahamu. Imekuwa ni salamu ya kitaifa, ikiamsha ari ya kuendelea kupambana katika kuijenga Tanzania yetu.

Ni salamu iliyobuniwa na kutambulishwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambaye Machi 19, 2024 alitimiza miaka mitatu madarakani tangu alipoapishwa kuwa Rais wa Awamu ya Sita.

Alichukua nafasi hiyo na kuwa Rais wa kwanza mwanamke Tanzania na Afrika Mashariki kufuatia kifo cha mtangulizi wake, Hayati Dkt. John Pombe Magufuli, aliyefariki Machi 17, 2021, akiwa madarakani.

Katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wake, sekta za Biashara, Uwekezaji na Viwanda zimeimarika kwa kiwango kikubwa.

BRELA inaendelea kutekeleza lake iliyokasimiwa (*ni Taasisi iliyokasimiwa jukumu*) la kusajili Kampuni, Majina ya Biashara, kutoa Leseni za Biashara kundi "A", kutoa Leseni za Viwanda, kusajili Hataza, Alama ya Biashara na Huduma. Aidha utoaji huduma umeboreshwa kwa kuweka mazingira wezeshi ya biashara nchini.

Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, Bw. Godfrey Nyaisa, anasema kuwa ufanisi wa kazi umeongezeka, akibainisha kwamba hilo linachagizwa na ari ya kujituma kwa wafanyakazi, kuwepo kwa uwiano wa asilimia



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Machi 19, 2024 ametimiza miaka mitatu madarakani.*

50 kwa 50 ya watumishi wanawake na wanaume, hali inayosaidia kuwepo ongezeko la sajili, leseni na ukusanyaji wa mapato na kufikiwa kwa malengo ya Taasisi.

Anasema kuwa katika kuhakikisha hali hiyo inakuwa endelevu, kila mtumishi wa BRELA anajengewa uwezo kumsaidia kufahamu misingi ya Taasisi, Dhima na Dira ili aweze kuhudumia wateja kwa weledi na kwa kiwango cha hali ya juu, hali inayoongeza hamasa kwa wananchi na wadau kurasimisha biashara zao na kuwa sehemu ya wachangiaji wa maendeleo ya taifa na pia kufanikisha malengo ya Wakala.

Bw. Nyaisa anataja vipaumbele ambavyo Taasisi imejiwekea kuwa ni pamoja na kuwa na mifumo imara na thabiti katika uendeshaji wa Wakala na kuutaja mfumo wa usajili wa *Online Registration* (ORS) na Tanzania National Business Portal (TNBP), ambayo inamwezesha mfanyabiashara kusajili biashara na kupata Leseni. Mifumo inawezesha uendeshaji ulio bora wa kitaasisi na mifumo mingine ambayo ipo ndani ya ofisi ambayo pia inawezesha nyaraka mbalimbali kuwa katika ubora. Mifumo hii tunaipata kutoka Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA) pamoja na Wizara ya Fedha.

Pili, kuboresha uhusiano baina na wadau mbalimbali wakiwemo wale ambao (baadhi) wamesaini hati za makubaliano ambao ni pamoja na FCC, TAKUKURU, COSOTA. Pia kufanya tafiti kwa kushirikiana na taasisi nyingine za utafiti kwa lengo la kuboresha Taasisi yetu.

Tatu, Wakala imefanya mapitio ya sheria mbalimbali ambazo zinasimamia utendaji kazi wa Taasisi. Sheria hizo ni pamoja na Sheria ya Leseni, Sheria ya Kampuni, ambapo imeanza na sheria mama ya kampuni ambayo kwa kushirikiana na Tume ya Kurekebisha Sheria wanafanya mapitio kwa ajili ya kufanyia marekebisho katika kanuni na kurekebisha maeneo ambayo yamekuwa yakilalamikiwa na wadau.

Sambamba na hilo Bw. Nyaisa amebainisha kuwa, katika kipindi hiki cha miaka mitatu ya uongozi wa Rais Samia ukusanyaji wa mapato umeongezeka kwa asilimia 12 na hii inatokana na uimarishwaji wa mifumo ambapo mtu anaweza kufanya usajili na kulipia kwa njia ya mfumo.

Aidha, BRELA imeendelea kuimarisha mahusiano baina yake na taasisi zingine kwa kuimarisha upatikanaji wa taarifa na kutolea mfano kwa kubadilishana taarifa kati ya Wakala na NIDA, FCC, VODACOM, Mabenki ya biashara. Kutokana na kujenga mahusiano mazuri taasisi hizo zina uwezo wa kupata taarifa wanazozihitaji kwa haraka na kwa wakati.

Pia imekuwa ikiunga mkono juhudi za Rais za kutaka wafanyabiashara wajengewe mazingira bora zaidi ya kufanya biashara zao kwa uhakika, BRELA imekuwa ikifanya kazi kwa kufuata miongozo na Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Katika kufanikisha hayo yote na kusonga mbele zaidi katika kuchagiza maendeleo ya Taifa, BRELA imerahisisha utoaji wa huduma zake kwani inatoa huduma zake kwa njia ya teknolojia ya mtandao kwa kutumia mifumo unayojulikana kama *Online Registration System* (ORS) na Tanzania National Business Portal (TNBP) , mifumo rahisi iliyoenea nchi nzima.

Kutokana na mifumo hiyo, Mtanzania yeyote anaweza kusajili Kampuni, Jina la Biashara, Alama za Biashara na Huduma, kupata leseni ya biashara kundi "A" na leseni ya kiwanda kwa njia ya mtandao mahali popote alipo.




Mifumo hiyo imeleta mageuzi kwa kuwa unahakikisha wateja wanapata taarifa zao zote. Hivyo, wateja wote wanaweza kupata taarifa zao kwenye mfumo bila mhusika kuhitajika kufika ofisi za BRELA. Kwa kuwa huduma zote za Wakala zinatolewa kwa njia ya mtandao.

Tunapoadhimisha miaka mitatu tangu Rais Mhe. Dkt. Samia alipoingia madarakani, yapo mengi ya kujivunia, kubwa zaidi ni BRELA kuendelea kutekeleza majukumu yake yote kidigitali. Wakala imeendelea na jitihada zinazoendana na kasi ya kidunia, mipango mbalimbali, ikiwemo Dira ya Maendeleo ya Taifa, Mpango wa Miaka Mitano wa Taifa na Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020, na hakuna mashaka kwamba inaendelea kutekeleza wajibu wake kidijitali.

BRELA imeweza kuandaa na kufanya mkutano na wadau wake kwa mara ya kwanza ambapo iliwakutanisha kwa lengo la kuwatambua na kuwashirikisha Dira, Dhima na Malengo, sambamba na kusikiliza kero zinazowakabili na kufanya majadiliano ya pamoja ya namna ya kuzitatua.

Mkutano huo ulifanyika sambamba na maonesho ya huduma za wadau ya liyowahusisha wafanyabiashara, wajasiriamali wakubwa na wadogo, waandishi wa habari pamoja na taasisi za serikali zinazowezesha ukuaji wa biashara na uwekezaji nchini kwa lengo la kutangaza huduma zao kwa wananchi na kutatua changamoto za wafanyabiashara.

Takwimu zinaonyesha kuwa katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita kumekuwa na ongezeko la usajili wa kampuni na majina ya biashara kama inavyobainishwa na wataalam wa BRELA.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Usajili wa Kampuni na Majina ya Biashara wa BRELA, Bw. Isdory Nkindi, katika kipindi hiki cha miaka mitatu ya Awamu ya Sita ya uongozi wa Dkt. Samia Suluhu Hassan kumekuwa na ongezeko kubwa la usajili wa Kampuni na Majina ya Biashara kwa wafanyabiashara wa ndani na nje ya nchi. Hii ni kutokana na juhudi za Rais kuvutia wawekezaji, sambamba na mwamko wa wajasiriamali kusajili majina ya biashara zao kwa ajili ya kufanya biashara kuwa rasmi.

Hivi sasa BRELA imejipambanua zaidi kwa kwenda kutoa huduma mtaa kwa mtaa ili kuwajengea uwezo na kutoa elimu kwa wafanyabiashara wanaosajili biashara zao. Aidha, Taasisi hii inafanya kampeni hii katika mikoa yote ya Tanzania Bara ili kuwaelimisha wafanyabiashara kurasimisha biashara na ambapo mikoa sita imefikiwa - Mwanza, Mbeya, Arusha, Kilimanjaro, Dodoma na Dar es Salaam na kuendelea katika mikoa mingine.

Kwa sasa mwamko wa wafanyabiashara umekuwa mkubwa ambao unachangiwa na jitihada na hamasa inayotolewa na BRELA kwa wafanyabiashara kwa kurusha vipindi kupitia vyombo vya habari vya kitaifa vikiwemo mitandao na redio za kijamii (*community radios*). Hamasa na elimu imekuwa ikitolewa juu ya umuhimu na namna ya urasimishaji na uhuishaji wa biashara na Kampuni na upataji Leseni ya biashara kundi A.

Katika kipindi cha miaka mitatu, usajili umeongezeka ambapo mwaka 2021 Kampuni 10,862 zilisajiliwa; mwaka 2022 kampuni 13,756 na mwaka 2023 kampuni 15,964. Kwa jumla, kampuni zilizosajiliwa zimefikia 40,582 sawa na ongezeko la asilimia 76 ikilinganishwa na kampuni 23,166 zilizosajiliwa katika kipindi kati ya mwaka 2018 hadi 2020.

Kwa upande wa Majina ya Biashara, mwaka 2021 majina ya biashara 21,836, mwaka 2022 Majina ya biashara 25,507 yamesajiliwa na mwaka 2023 majina 29,517 na kufanya jumla ya majina ya biashara yaliyosajiliwa kuwa 76,860 sawa na ongezeko la asilimia 85 ikilinganishwa na Majina ya Biashara 41,414 yaliyosajiliwa katika kipindi kati ya mwaka 2018 hadi 2020.

Naye Mkurugenzi wa Miliki Ubunifu wa BRELA, Bi. Loy Mhando, anasema kuwa kurugenzi yake inayosimamia Sheria ya Alama za Biashara na Huduma pamoja na Sheria ya Usajili wa Hataza kwa maana ya kutoa ulinzi wa vumbuzi, katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Awamu ya Sita kurugenzi hiyo imeshuhudia mafanikio mbalimbali ikiwemo kuongezeka kwa maombi ya Alama za Biashara na Huduma pamoja na Hataza.

Hii inaonesha kwamba masuala ya miliki ubunifu na ubunfu kwa ujumla yanasaidia katika kutatua changamoto mbalimbali katika jamii, pia wamiliki wa Alama za Biashara na Huduma (Brand) wanaona umuhimu wa kutambulisha bidhaa zao katika soko.

Kwa kuwa Alama ya Biashara na Huduma ni nyenzo muhimu katika kuitambulisha bidhaa katika soko, hivyo bila kuweka nembo ama alama katika bidhaa inakuwa vigumu kwa walaji kutambua ubora, umaarufu ama utambulisho wa bidhaa husika kuwa ni ya nani.

Aidha, katika kipindi cha miaka hii mitatu takwimu zinaonesha kuwa mwaka 2021 Hataza 32 zilitolewa, mwaka 2022 Hataza 52na mwaka 2023 Hataza 76 na kufanya jumla ya Hataza 160 ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 33 ikilinganishwa na Hataza 120 zilizotolewa katika kipindi cha mwaka 2018 hadi 2020.

Kwa upande wa usajili wa Alama za Bishara na Huduma kwa mwaka 2021 jumla ya Alama 3,137 zilisajiliwa; mwaka 2022 Alama za Biashara na Huduma 3,607 na mwaka 2023 Alama na Huduma 3,860 na kufanya jumla ya Alama za Biashara na Huduma zilizosajiliwa kuwa 10,604, sawa na ongezeko la asilimia 23.

BRELA kupitia Kurugenzi ya Miliki Ubunifu imeendelea kutoa elimu juu ya umuhimu wa wabunifu kulinda na kunufaika na bunifu zao na kuzuia watu wengine kutumia bunifu za wenzao. Pia Nyanja ya Miliki Ubunifu ina sura ya kimataifa hivyo BRELA imejenga zaidi mahusiao ya kimataifa na kikanda kwa kujenga uwezo. Pia inatoa mafunzo na ulezi na uatamizi (incubation) kwa wajasiriamali ili waweze kuhakikisha bunifu zao zinalindwa na kutambulika.

Naye Mkurugenzi wa Leseni wa BRELA, Andrew Mkapa, ambaye Kurugenzi yake inasimamia sheria mbili; Utoaji wa Leseni za Biashara kundi “A”, Utoaji wa Leseni za Viwanda na Utoaji wa vyeti vya Usajili wa Kiwanda, anasema katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Dkt. Samia Suluhu Hassan mwaka 2021 zilitolewa Leseni za Biashara kundi “A” 12,574, mwaka 2022 Leseni 14,263 na waka 2023 leseni 18,241 na kufanya jumla ya Leseni 45,078, sawa na ongezeko la asilimia 26 ikilinganishwa na Leseni 35,739 zilizotolewa katika kipindi kati ya mwaka 2018 hadi 2020.

Katika eneo la utoaji wa Leseni za Viwanda na vyeti vya usajili wa Viwanda, pia kumekuwepo

na ongezeko la asilimia 56, ambapo mwaka 2021 Leseni 183 zilitolewa, mwaka 2022 Leseni 163 na mwaka 2023 Leseni 285, na hivyo kufanya jumla ya Leseni za viwanda 631 zilitolewa kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mafanikio haya yanatokana na juhudi za Rais kufungua milango na njia za kiuchumi, pamoja na kuwepo kwa sera rafiki katika ufanyaji biashara na uwekezaji katika sekta ya viwanda. Wafanyabiashara wamepata mwamko wa kusajili viwanda vyao ama kuvikatia leseni kama sheria inavyoelekeza na kuboreshwa kwa mazingira ya biashara.

Pia kumekuwa na utaratibu wa kufanya ukaguzi wa mara kwa mara katika mikoa yote kwa lengo la kuwakumbusha wafanyabiashara kuendesha biashara kulingana na sheria. Taasisi imeweza kufanya mapitio na kuboresha sheria zote mbili ambazo zimefikishwa Bungeni ili ziboreshwe kuendana na wakati na kuweka mazingira bora ya biashara.

BRELA inaendelea kufanya maboresho na kujiimarisha ili kutoa huduma zake kuendana na mapinduzi ya nne ya viwanda kwa matumizi ya teknolojia.

Azma yake ni kuhakikisha inakuwa Taasisi ya mfano katika utoaji wa huduma za usajili wa biashara na utoaji wa leseni kikanda, jambo ambalo tayari daliili zimeanza kuonekana kwani hivi karibuni ilipata ugeni kutoka Jamhuri ya Burundi na Sudan ya Kusini kwa ajili ya kujifunza jinsi ya kutoa huduma kwa njia ya mtandao.

# Kijaji aziagiza taasisi zinazotoa leseni kukagua viwanda vinavyozalisha mabati

**Na Mwandishi Wetu**

Waziri wa Viwanda na Biashara, Dkt. Ashatu Kijaji, amezitaka taasisi zinazohusika na utoaji leseni, ikiwemo BRELA, Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na Wakala wa Vipimo (WMA) kufanya ukaguzi kwa viwanda vyote nchini vinavyozalisha mabati na bidhaa nyingine ili kujiridhisha iwapo bidhaa hizo zinakidhi vigezo vilivyoainishwa na kukubalika na serikali.

Waziri Kijaji alitoa wito huo Februari 22, 2024, jijini Dodoma wakati alipofanya ziara katika viwanda vya kuzalisha mabati vya ALAF na Herosean Interprises inayozalisha mabati ya DRAGON ikiwa ni utekelezaji wa maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan kuhakikisha bidhaa zinazozalishwa na viwanda hapa nchini zinaboreshwa.

Dkt. Kijaji akiwa kwenye kiwanda cha Herosean Interprises alibaini uwepo wa bidhaa nyingine ambazo hazihusiani na malengo halisi ya leseni iliyotolewa na BRELA ikiwemo majokofu, PVC, vigae na *gypsum board* na kuziagiza taasisi zinazohusika na suala hilo zibaini ukweli wake.

Vile vile, Dkt. Kijaji alivitaka viwanda vinavyozalisha mabati nchini kuuza kwa bei rafiki ili kunufaisha wanunuzi kwa makundi yote.

Pia aliwataka Watanzania kuendelea kujenga kwa wingi kwa vile bei za mabati kwa Tanzania ni nafuu ikilinganishwa na nchi nyingine za Afrika Mashariki.



*Waziri wa Viwanda na Biashara, Dkt. Ashatu Kijaji,akipata maelezo jinsi bati zinavyotengenezwa, wakati alipofanya ziara katika viwanda vya ALAF na kiwanda cha Dragon jijini Dodoma, Februari 22, 2024.*

# Burundi, Sudan Kusini waelimishwa kuhusu utoaji huduma kwa njia ya mtandao

**Na Christina Njovu**

Maafisa kutoka Burundi na Sudan ya Kusini kuanzia Machi 25, 2024 walifanya ziara ya siku tatu nchini Tanzania wakiwa wageni wa BRELA ili kujifunza namna Taasisi hiyo inavyotoa huduma za urasimishaji wa biashara kwa njia ya mtandao. Mafunzo yalifanyika ofisi za BRELA jijini Dar es Salaam.

Akifungua mafunzo hayo, Kaimu Mkurugenzi Idara ya Maendeleo ya Biashara kutoka Wizara ya Viwanda na Biashara, Bw. Sempeho Manongi, ambaye alimwakilisha Katibu Mkuu wa Viwanda na Biashara, alisema kuwa lengo la mafunzo hayo ni kuwaelimisha wawakilishi hao jinsi ya kutumia mifumo ya usajili ili wakatumie ujuzi huo kuanzisha na kuendeleza mifumo kama hiyo kwenye nchi zao.

"Katika moja ya mambo makubwa ambayo serikali imefanya ni kuunganisha mfumo mmoja wa kuwezesha kusajili biashara na kupata leseni, uliowezesha kufanya vizuri zaidi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na kuzivutia nchi za Sudan Kusini na Burundi kuja kujifunza," alisema Bw. Manongi.

Kwa upande wake Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, Bw. Godfrey Nyaisa, alieleza kufurahishwa kwake na ujio wa ugeni huo wa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kuiona Tanzania kupitia taasisi ya BRELA kuwa imepiga hatua katika matumizi ya mfumo ya kutoa huduma kwa njia ya mtandao.

Alisema ziara hiyo inaonesha wazi kuwa kazi kubwa inafanyika katika uwezeshaji na urasimishaji wa biashara nchini.

"Sisi tutawapitisha na kuwaonesha mifumo yetu hatua kwa hatua namna mfanyabiashara anavyosajili hadi afisa anavyochakata maombi. Mbali na hayo tunatarajia kutengeneza mashirikiano ya kufanya kazi ili sisi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki tuweze kuongea lugha moja," alieleza Bw. Nyaisa.

Naye Mwakilishi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki anayeshughulikia masuala ya uwekezaji, Bw. Charles Omusama, alisema nchi hizi mbili zipo kwenye mchakato wa kuanza kutoa huduma za usajili kwa njia ya mtandao, hivyo Tanzania imeonekana ni nchi iliyopiga

# Kijaji aziagiza taasisi zinazotoa leseni ...

Kwa nyakati tofauti, Bw. Herry Jailos, Afisa Huduma kwa Wateja katika kiwanda cha ALAF, na Bw. Boniface Lekwasa, Afisa Masoko wa kiwanda cha Dragon, waliishukuru serikali kwa kufanya ziara na kubaini changamoto zinazowakabili ikiwemo ukosefu wa masoko kutokana na uwepo wa wazalishaji wengi wa bidhaa hiyo.





*Waziri wa Viwanda na Biashara Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji akipata maelezo kuhusu uzalishaji wa mabati alipotembelea kiwanda cha ALAF na kiwanda cha Dragon jijini Dodoma, Februari 22, 2024.*

# Burundi, Sudan Kusini waelimishwa ...

hatua katika utoaji wa huduma kwa kutumia mifumo huo.

Aidha, Kaimu Msajili Mkuu wa Kampuni za Biashara kutoka Wizara ya Sheria nchini Sudan ya Kusini, Bw. Madol Anyuat, alisema kuwa wamekuja Tanzania kwa ajili ya ziara ya mafunzo kwa vitendo ili waweze kuona namna mifumo ya sajili inavyofanya kazi ili watakaporudi nchini kwao wakachukue hatua ya kuanzisha mifumo ya kusaidia ukuaji wa sekta ya biashara.

Naye Bi. Alida Mugisha, alieleza kuwa Burundi imeanza kutumia mifumo ya usajili mwaka 2022 ingawa bado wanakumbana na changamoto mbalimbali.

Alisema Tanzania imepiga hatua kubwa na kwamba ziara yao itawajengea uwezo ili waboreshe mifumo ya usajili kwa mtandao katika nchi yao.

Mafunzo hayo yaliyoanza Machi 25 yaliendeshwa kwa siku tatu sambamba na mafunzo kwa vitendo pamoja na kutembelea baadhi ya wadau wakubwa wanaotumia huduma za BRELA.



*Ujumbe wa wawakilishi kutoka Burundi na Sudan Kusini wakiwa katika picha ya pamoja na watumishi wa BRELA walipotembelea Taasisi hiyo kwa ajili ya kujifunza jinsi mfumo wa wa BRELA wa usajili kwa njia ya mtandao (ORS) unavyofanyakazi*



*Afisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni Bw. Godfrey Nyaisa akitoa maelezo kuhusu mfumo wa usajili kwa njia ya mtandao unavyofanya kazi wakati wa mafunzo kwa ujumbe wa wawakilishi kutoka Burundi na Sudan ya Kusini walipotembelea Ofisi za Wakala jijini Dar es Salaam, 2024*

# Kamati ya Bunge yasifu utendaji kazi wa BRELA

**Na Theresa Chilambo**

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo imeridhishwa na ufanisi wa utendaji kazi, ukuaji na mageuzi makubwa yaliyofanywa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), ikizingatiwa kuwa kigezo cha kwanza cha ufanyaji biashara Tanzania ni kupitia BRELA.

Kauli hiyo ilitolewa na Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Deodatus Mwanyika (Mb), baada ya wajumbe wa Kamati wakati wa mafunzo yaliyotolewa na BRELA Februari 11, 2024 jijini Dodoma.

“Tumeyaona, tumeyasoma, tumeyasikia na kuyahoji, zaidi tumeridhika sana na yale yanayofanyika ndani ya BRELA, mathalani, ukitaka kuanzisha kampuni ndani ya siku mbili hadi tatu unapatiwa cheti chako ndani ya mfumo. Vivyo hivyo, kwa upande wa jina la biashara pia ni siku moja au saa tu endapo utakuwa umekamilisha nyaraka zote zinazohitajika. Baadhi ya wabunge wameshuhudia kuwa wameweza kusajili kwa muda mfupi, hivyo ni viashiria tosha kuwa Taasisi imejipanga na imeimarisha mifumo yake,” alieleza Mwanyika.

Alimpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa jitihada anazozifanya za kuweka mazingira mazuri ya biashara ili Tanzania iweze kusonga mbele kwa kuwa na wawekezaji wa ndani na nje ya nchi.

Katika muktadha huo, kupitia BRELA tumeona hatua kubwa iliyopiga, maana huo ndio uhai wa mazingira ya biashara, alisisitiza Mwanyika.

Naye Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exhaud Kigahe, alisema kuwa wizara ina jukumu la kuhakikisha

wananchi wanafahamu kazi zinazotekelezwa na serikali kupitia taasisi zilizo chini yake, ambao ndiyo wadau wakubwa.

"Tunapokutana nanyi wawakilishi wao tunapata mrejesho kwa yale ambayo tunaweza kufanya vizuri kupitia BRELA; taasisi ambayo ipo chini yetu, na pia kuona namna gani tunaenda kuchukua mawazo ambayo wananchi wangependa kuona taasisi hii inafanya, hasa katika usajili na utoaji wa leseni bila ukiritimba au urasimu usio na lazima. Zaidi ni kutoa elimu kwa wananchi ukizingatia maeneo mengi yanahitaji wafanyabiashara wanaotambulika rasmi," alifafanua Kigahe.

Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, Bw. Godfrey Nyaisa, aliwahakikishia wajumbe wa kamati kuwa mbali na kuwaeleza kuhusu majukumu ya taasisi, BRELA inaendelea kuboresha utendaji wake ikiwemo kufanya marekebisho ya Sheria ya Kampuni iendane na mahitaji yaliyopo ili kwenda na wakati katika kuhudumia wafanyabiashara na kuhakikisha biashara zinakua.

BRELA ilitoa mafunzo kwa Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, ili kupata uelewa zaidi wa namna inavyotekeleza majukumu yake.

Hii ni kutokana na ukweli kwamba wabunge hao wana jukumu la kikatiba la kuisimamia na kuishauri Serikali. Kwa hiyo wanapaswa kujengewa uwezo ili wawe na ufahamu wa kutosha wa namna taasisi zinavyofanya kazi na kufahamu changamoto zao pamoja kuzipatia ufumbuzi.



*Mkurugenzi wa Leseni Bw. Andrew Mkapa akitoa ufafanuzi kuhusu marekebisho ya Sheria ya Kampuni wakati wa mafunzo kwa wajumbe wa kamati ya Kudumu ya Bunge yaliyofanyika Februari 11, 2024 jijini Dodoma*



*Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara Mhe. Exhaud Kigahe (aliyesimama) akitoa ufafanuzi kuhusu jukumu la Wizara yake wakati wa mafunzo kwa wajumbe wa Kamati ya Bunge yaliyoandaliwa na BRELA, kushoto kwake ni Katibu Mkuu wa Wizara hiyo Dkt. Hashil Abdallah*



*Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo wakisimama kwa dakika moja kabla ya kuanza mafunzo kufuatia kifo cha aliyekuwa Rais wa Awamu ya Pili wa jamhuri ya Muungano wa Tanzania Hayati Ali Hassan Mwinyi aliyefariki dunia Februari 29, 2024*



# Watumishi BRELA wajengewa uwezo kuhusu majukumu ya ARIPO

**Na Lugano Mwakyombe**

Watumishi wa BRELA, Kurugenzi ya Miliki Ubunifu, wamejengewa uwezo kuhusu majukumu ya Shirika la Miliki Ubunifu Kanda ya Afrika (African Regional Intellectual Property Organization - ARIPO) pamoja na uchakataji wa Hataza.

Mafunzo hayo ya siku moja yalifanyika Januari 18, 2024 mwaka huu katika ofisi za BRELA jijini Dar es Salaam.

Katika mafunzo hayo, Mkuu wa Kitengo cha Utafiti na Uchambuzi wa Hataza kutoka ARIPO, Bi. Flora Mpanju, alielezea kuhusu shughuli na Itifaki zinasosimamiwa na Taasisi hiyo.

Bi. Mpanju alizitaja Itifaki hizo kuwa ni Itifaki ya Arusha ya ulinzi wa aina mpya za mbegu za mimea, Itifaki ya Kampala ya usajili wa hiarı wa hakimiliki na hakishiriki, Itifaki ya Banjul ya ulinzi wa alama, Itifaki ya Harare ya hataza na maumbo bunifu, pamoja na Itifaki inayohusu ulinzi wa masuala ya maarifa asili na matamko ya kale.



*Mkuu wa Kitengo cha Utafiti na Uchambuzi wa Hataza wa ARIPO, Bi. Flora Mpanju (kushoto) akimsikiliza Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu, Bi. Loy Mhando, wakati wa ufunguzi wa mafunzo kuhusu majukumu ya ARIPO yaliyofanyika Januari 18, 2024 katika ofisi za BRELA, jijini Dar es Salaam.*

Pia alipongeza juhudi zinazofanywa na BRELA katika kuhakikisha inawafikia wadau wake na kuwapatia elimu kuhusu ulinzi wa bunifu mbalimbali kwa kuzingatia sheria za nchi, miongozo ya ARIPO na Shirika la Miliki Ubunifu Duniani (WIPO).

“Nimefuatilia kwa karibu kazi mnazofanya, niwapongeze na salamu hizi zimfikie Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, kuwa mnafanya kazi kubwa na juhudi zenu zinaonekana kote, mfano tulipoona ushiriki wenu katika Maonesho ya Kimataifa ya Biashara ya Sabasaba tulijifunza mengi na msimu uliopita mlikuwa na banda maalum la masuala ya Miliki Ubunifu ni hatua za kujivunia,” alisema Bi. Mpanju.

Aliwahakikishia washiriki kuwa ARIPO itaendelea kushirikiana na BRELA ili kuhakikisha bunifu mbalimbali zinalindwa kwa kuwapa elimu wadau juu ya umuhimu wa kulinda bunifu zao kwa manufaa ya wavumbuzi na taifa kwa ujumla.

Akitoa neno la shukrani kwa niaba ya Afisa Mtendaji Mkuu, Kaimu Mkurugenzi wa Miliki Ubunifu Bi. Loy Mhando, alimshukuru Bi. Mpanju kwa ujio wake na kuahidi kuwa Taasisi itaendelea kushirikiana na ARIPO ili elimu na ulinzi wa bunifu ufanyike kwa viwango vinavyotakiwa.



*Watumishi wa BRELA Bi. Grace Umoti na Bw. Abdukarim Ally wakimsikiliza Bi. Flora Mpanju (hayupo pichani) akitoa mafunzo elekezi kuhusu shughuli na Itifaki zinazosimamiwa na ARIPO*

# Nyaisa awapongeza wafanyakazi wanawake kwa uaminifu wa utendaji kazi

**Na Christina Njovu**

Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA) Bw. Godfrey Nyaisa, Machi 8, 2024 aliwapongeza watumishi wanawake kwa kufanya kazi kwa uaminifu na ufanisi uliowezesha kufikiwa kwa malengo ya Taasisi kiutendaji na katika ukusanyaji wa mapato.

Alitoa pongezi hizo wakati wa hafla ya kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani iliyofanyika katika viwanja vya Ofisi za BRELA jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na watumishi wanawake,, Bw. Nyaisa alibainisha kuwa BRELA ina uwiano sawa wa wafanyakazi wanawake na wanaume kwa asilimia 50 kwa 50 na kwamba uwepo wa wanawake katika ofisi, uaminifu na ufanisi katika kazi unaongezeka zaidi.

"Niwapongeze sana wanawake mmekuwa mkitulia maofisini na kufanya kazi, hivyo utendaji kazi unaonekana, na makusanyo ya mapato ni mazuri ukilinganisha na ofisi nyingine. Utendaji kazi huu ni lazima uwe endelevu usiwe wa matukio tu," alisisitiza Bw. Nyaisa.

Alisema kuwa siku zote "tunasema akina mama wanaweza wakijiongeza" na kutoa wito kwao kuelezana ukweli ikiwa mmojawapo anafanya kazi chini ya kiwango anawarudisha wengine nyuma na kufifisha maendeleo ya Taasisi.

Naye Kaimu Mkurugenzi wa Miliki Ubunifu, Bi. Loy Mhando, akimkaribisha Afisa Mtendaji Mkuu kuzungumza na wafanyakazi wanawake wa BRELA alimhakikishia kuwa "tukiwa ni wanawake tutaendelea kufanya kazi kwa juhudi ili tusirudishe nyuma mipango yote ya Taasisi na kuwezesha iendelee kusonga mbele."

Alisistiza kwamba ili uwekezaji kwa mwanamke uweze kufanyika ni lazima kuwa tayari kwenda na mabadiliko bila kusubiri kukumbushwa bali kuwa na maamuzi na mambo yote yatafanikiwa.




*Watumishi wanawake wa BRELA wakiwa wamebeba bango kuelekea kwenye maandamano ya kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani Machi 8, 2024, Mjimwema, Kigamboni jijini Dar es Salaam*

# Wanawake BRELA waunga mkono juhudi za Rais kutangaza utalii

**Na Sheila Mfunami**

Wanawake wa BRELA katika kuhitimisha maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani mwaka huu walipata fursa ya kutembelea Hifadhi ya Taifa ya Nyerere ikiwa ni kuunga mkono juhudi za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kutangaza utalii, fursa za biashara na uwekezaji.

BRELA ilitumia nafasi hiyo ikiwa ni sehemu ya kuhamasisha utalii wa ndani pamoja na kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani ambayo huadhimishwa kila mwaka ifikapo Machi 8.

Kabla ya kutembelea Hifadhi ya Taifa ya Nyerere, watumishi wanawake wa BRELA walishiriki katika maandamano ambayo kwa Mkoa wa Dar es Salaam yalifanyika katika Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni kwenye viwanja vya Mji Mwema na kupokelewa na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila.



*Wanawake kutoka Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni wakiwa ndani ya treni ya Shirika la Reli la TAZARA kuelekea Hifadhi ya Taifa ya Nyerere ikiwa ni kuunga mkono juhudi za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika kutangaza utalii, fursa za biashara na uwekezaji pamoja na kuadhimisha siku ya Wanawake Duniani Machi 9, 2024.*

## Wajasiriamali wakumbushwa umuhimu wa Miliki Ubunifu katika soko la huduma

**Na Njwaba Mwaijibe**

Wajasiriamali wamekumbushwa kuhusu umuhimu wa kusajili bunifu zao ili ziweze kuwanufaisha katika soko la biashara na huduma.

Huo ni wito uliyotolewa na BRELA Februari 15, mwaka huu, wakati wa semina iliyowakutanisha wajasiriamali mbalimbali kutoka katika viunga vya Jiji la Dar es Salaam iliyofanyika katika Ukumbi wa Hoteli ya Golden Tulip.

Wajasiriamali hao ambao walipatiwa mafunzo mbalimbali kutoka Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) walielezwa jinsi ambavyo Miliki Ubunifu ina mchango katika kukuza biashara na huduma.



*Afisa Usajili wa BRELA Bw. Stanislaus Kigosi akiwasilisha mada kwa wajasiriamali kutoka SIDO jijini Dar es Salaam*



*Baadhi ya wajasiriamali kutoka SIDO wakishiriki mafunzo kuhusu mchango wa miliki Ubunifu.*




*Wanawake kutoka Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni wakiwa katika picha ya pamoja na madereva wanawake wa treni kutoka Shirika la Reli laTAZARA baada ya kuwasili katika Hifadhi ya Taifa ya Nyerere ikiwa ni kuunga mkono juhudi za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kutangaza utalii, fursa za biashara na uwekezaji pamoja na kuadhimisha siku ya Wanawake Duniani Machi 9, 2024..*



*Wanawake kutoka Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni wakipata elimu juu ya mnyama kiboko na mamba kutoka kwa Askari wa Mamlaka ya Hifadhi za Taifa (TANAPA), Agusti Chuwa, walipotembelea Bwawa lililopo ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Nyerere.*

# BRELA, TPHPA kuimarisha ushirikiano

**Na Njwaba Mwaijibe**



*Ujumbe wa watumishi kutoka BRELA wakiwa pamoja na uongozi wa TPHPA kujadili kuhusu kuimarisha ushirikiano baina ya taasisi hizo walipokutana tarehe 19 Februari, 2024 katika Ofisi za TPHPA jijini Arusha.*

BRELA na Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania (TPHPA) ni taasisi zilizokubaliana kuimarisha ushirikiano ili kulinda wamiliki wa Alama za Biashara na huduma za wazalishaji na wauzaji wa viuatilifu nchini.

Makubaliano hayo yalifikiwa katika mazungumzo baina ya Kaimu Mkuu wa Sehemu ya Alama za Biashara na Huduma wa BRELA, Bw. Seka Kasera, na Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TPHPA, Dkt. Osmundi Ndomba, akiwa ameambatana na watumishi wengine katika ofisi za Mamlaka hiyo jijini Arusha.

Kaimu Mkuu wa sehemu ya Alama za Biashara na Huduma wa BRELA Bw. Kasera, aliambatana na watumishi wengine wa BRELA katika ofisi za TPHPA kwa ajili ya kikao kazi cha siku mbili ili kubaini maeneo yenye mwingiliano wa kisheria na kiutendaji.

Bw. Kesera alisema lengo la mazungumzo na TPHPA ni kuona namna ya kupunguza migogoro inayotokea kwa wazalishaji wa viuatilifu nchini kuhusu umiliki wa Alama za Biashara na Huduma.

Alisema kuwa wazalishaji wa viatilifu nchini wamekuwa wakitumia Alama za Biashara kutambulisha bidhaa zao sokoni, hivyo ni vyema kukawa na uelewa mpana wa namna ambayo wanaweza kulindwa kwa mujibu wa sheria.

Aliongeza kuwa TPHPA inasajili viuatilifu nchini ni vyema kukawa na ushirikino na BRELA ili kuongeza upatikanaji wa taarifa ambazo zitawalinda wamiliki halali wa Alama za Biashara ambazo zimesajiliwa BRELA.

“BRELA na TPHPA si mara ya kwanza kukutana, hii ni mara ya tatu na sasa tunaona umuhimu wa kuwa na ushirikino zaidi katika utendaji kazi wetu ninyi kama Mamlaka inayosajili viuatilifu na sisi BRELA ambao tuna jukumu la kurasimisha Biashara nchini ili kuwa na uelekeo wa pamoja katika kulinda na kukuza biashara,” alisema Bw. Kasera.

Alifafanua kwamba Alama za Biashara na Huduma ambazo hutumika katika bidhaa mbalimbali, ikiwemo viuatilifu, zinapaswa kuwa zimesajiliwa BRELA ili kumlinda mmiliki halali wa bidhaa na kuzuia kutumiwa na watu wengine pasipo ridhaa ya mmiliki.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa TPHPA allipongeza BRELA na kuomba kufikisha salamu kwa Afisa Mtendaji Mkuu wake kwa uamuzi wa kuandaa kikao hicho ambacho kitatoa mwanga, kuongeza ushirikino na kukuza utendaji kazi baina ya taasisi hizo mbili.

Kikao kazi hicho cha siku mbili (2) kilichoanza Februari 19, 2024, kilihusisha pia utoaji elimu kuhusu huduma zinazotolewa na BRELA na mchakato wa urasimishaji wa biashara, na majadiliano katika maoneo ya ushirikiano baina ya taasisi hizo.




*Afisa Usajili Mwandamizi wa BRELA Bw. Seka Kasera akieleza kuhusu majukumu ya BRELA wakati wa kikao cha pamoja na uongozi wa TPHPA ili kubaini na kuainisha maeneo ya kuimarisha ushirikiano baina yao.*

# BRELA, TMDA kuimarisha ushirikiano katika utoaji huduma

**Na Gloria Mbilimonywa**

Taasisi mbili za BRELA na Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) Februari 29, 2024 zilifanya kikao kujadili ushirikiano ili kurahisisha zaidi utoaji wa huduma kwa wadau wao.

Akizungumza wakati wa kutambulisha ujumbe wa BRELA kwa Mkurugenzi wa Dawa za Binadamu na Mifugo wa TMDA, Bw. Yona Mwalwisi, Msajili Msaidizi Mkuu wa BRELA Bw. Seka Kasera, alisema kuwa mazungumzo hayo yataleta tija na ufanisi baina ya taasisi hizo mbili ikiwa ni pamoja na kuondoa migogoro ya wamiliki wa Alama za Biashara na wamiliki wa majina ya dawa.



*Afisa Vifaa Tiba kutoka Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba, Bi. Rose Maingu, akitoa mawasilisho kuhusu majukumu ya TMDA, hususan taratibu za usajili bidhaa za dawa na vifaa tiba kwa maafisa wa BRELA kwenye kikao kazi baina ya taasisi hizo mbili Februari 29, 2024, kwenye ofisi za BRELA jijini Dodoma*

Alisema BRELA na TMDA watakuwa na majadiliano ya pamoja ambayo yatawakutanisha wataalam kutoka taasisi hizo kwa ajili ya kuangalia na kubaini kwa pamoja maeneo ya kisheria na ya kiutendaji yenye kuonekana kuwepo kwa mwingiliano wa majukumu na kuweka mikakati ya pamoja ya kuondokana na mkanganyiko na mwingiliano huo ili kurahisisha utoaji wa huduma hasa katika sajili za Alama za Biashara na Huduma na utekelezaji wa usajili na usimamamizi wa vifaa tiba na dawa mbalimbali.

Bw. Kasera alifafanua kwamba kikao kazi hicho baina ya BRELA na TMDA ni mwendelezo wa utekelezaji wa mpango kazi wa kuimarisha ushirikiano na taasisi za udhibiti nchini ili kuondoa changamoto, hususan za kisheria ambazo zimekuwa zikijitokeza wakati na baada ya utoaji wa huduma.




*Maafisa wa BRELA wakiwa katika picha ya pamoja na maafisa kutoka Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) baada ya kuhitimisha kikao kazi kwa siku ya kwanza cha kujadili ushirikiano baina ya taasisi hizo mbili Februrari 29, 2024, katika ofisi za BRELA jijini Dodoma.*

## BRELA, TMDA ...

"Katika kutelekeza majukumu yetu tunapaswa kushirikiana ili kutoa huduma za haraka na rafiki ukizingatia umuhimu wa taasisi hizi, TMDA mkisimamia dawa na vifaa tiba na BRELA tukiwa upande wa urasimishaji wa biashara, ambapo eneo la kufanikisha zaidi ni Alama za Biashara na Huduma, sambamba na vumbuzi mbalimbali zinazohusiana na dawa na vifaa tiba ziweze kulindwa kisheria ili tunufaike kwa pamoja kama nchi," alisisitiza Bw. Kasera.

Aliongeza kuwa BRELA na TMDA katika kikao hicho watapitia maeneo yote yenye mwingiliano kimajukumu na kuyaweka sawa ili kumwondolea usumbufu mteja pale anapotaka huduma; na hii itachochea uwekazaji zaidi.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Dawa za Binadamu na Mifugo, Bw. Mwalwisi, alimshukuru Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA kwa kuibua wazo hili ambalo litachangia katika kujenga mazingira rafiki kwa wafanyabiashara na wawekezaji, huku akisisitiza kuwa kikao kazi kama hicho ni muhimu kwa taasisi na taifa na utekelezaji wa makubalino utazaa matunda zaidi kwa kuondoa kero na kuleta umoja katika kufanya kazi.

Kikao kazi baina ya BRELA na TMDA ambacho kilihitimishwa Machi 1, 2024, kilitarajiwa kubaini na kuainisha maeneo ya ushirikiano ambayo yatasaidia katika kuandaa hati ya makubaliano ya ushirikiano (MoU) baina ya taasisi hizo mbili.

Wajumbe walikumbushwa kwamba hivi karibuni kilifanyika kikao kazi kama hicho jijini Arusha kati ya BRELA na TPHPA ambapo walijadili na kufanya mashauriano ambayo yatarasimishwa na Hati ya Makubaliano (MoU) ambayo pia imepangwa kusainiwa hivi karibuni na pande mbili husika.

# Mawakili, wafanyabiashara wafundishwa dhana ya wamiliki manufaa

**Na Christine Njovu**

Mawakili na wafanyabiashara nchini wametakiwa kuwabaini watu watakaojihusisha na vitendo vya uhalifu wa kifedha kwa kuwa vinakwamisha maendeleo ya taifa.

Katibu Tawala Msaidizi wa Mkoa wa Arusha anayesimamia Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Bw. Frank Mmbando, alitoa wito kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Arusha wakati akifungua kikao kazi baina ya BRELA na wadau kilichofanyika Jijini Arusha Februari 27 mwaka huu.

"Serikali inatambua kuwepo kwa changamoto za taarifa za baadhi ya wamiliki wa Kampuni ambao wanaweza kutumia Kampuni zao kukwepa kodi, kupitisha fedha haramu, kujihusisha na ufadhili wa vitendo vya ugaidi na ndio maana BRELA ilikutana na wawakilishi wa taasisi za uchunguzi na mamlaka za udhibiti ili kushauriana jinsi ya kukabiliana na changamoto hii ambayo inaleta taswira isiyo nzuri kwa wafanyabiashara nchini," alisema Bw. Mmbando.

Bw. Mmbando aliiongeza kuwa BRELA imeona umuhimu mkubwa wa kutoa elimu baada ya mabadiliko ya Sheria ya Fedha ya Mwaka 2020 iliyopitisha marekebisho kwenye Sheria ya Kampuni Sura 212. Marekebisho hayo ni pamoja na Kanuni za Wamiliki Manufaa wa Kampuni na Kanuni za Majina ya Biashara (Umiliki Manufaa) za Mwaka 2023 na Kanuni zake zilizopitishwa na waziri mwenye dhamana na biashara nchini.

Aliwasihi mawakili na wafanyabiashara hao waendelee kuwa mabalozi wazuri na kuwa jicho la serikali kwa kusaidia kuwafichua wale watakaobainika kujihusisha na vitendo kama hivyo kwa sababu vinakwamisha maendeleo ya taifa.

Alitoa rai pia kwa waandishi wa habari waliohudhuria warsha










*Baadhi ya washiriki wakimsikiliza Katibu Tawala Msaidizi wa Mkoa wa Arusha anayesimamia Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Bw. Frank Mmbando, (hayupo kwenye picha) akifungua kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa mafunzo ya siku moja kuhusu dhana ya wamiliki manufaa yaliyofanyika jijini Arusha.*

# Wahadhiri, wanafunzi TIA wahamasishwa kubobea katika fani ya Miliki Ubunifu

**Na Sheila Mfunami**

Wahadhiri na wanafunzi wa Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA) wamehamasishwa kuchagua maeneo ya kubobea katika taaluma ya kisayansi ili waweze kuandika maandiko mbalimbali ya maombi ya Hataza na Miliki Ubunifu.

Wito huo ulitolewa na Afisa Sheria kutoka BRELA, Bw. Andrew Malesi, wakati akitoa elimu ya Miliki Ubunifu chuoni hapo Februari 5, 2024, jijini Dar es Salaam.

Bw. Malesi alishauri kwamba ni vyema wanafunzi wa kada mbalimbali wakaona umuhimu wa kushiriki mafunzo kama hayo kwa sababu maisha ya binadamu ya kila siku yanazungukwa na kazi za Miliki Ubunifu ambazo kimsingi ni moja ya vyanzo vya mapato kwa wabunifu na watumiaji wa kazi za Miliki Ubunifu.

"Mtu akiwa na uelewa wa Miliki Ubunifu atajua namna bora ya kulinda ubunifu wake na namna bora ya kuingiza ubunifu wake kwenye soko la ndani na nje," alisema Bw. Malesi.

Naye Afisa Usajili wa BRELA, Bw. Stanislaus Kigosi, alisema TIA inafanya tafiti nyingi ambazo matokeo yake yanaweza kufanyiwa mchakato wa kuwa bidhaa au namna ya kutengeneza vitu mbalimbali.



*Washiriki wa mafunzo ya Miliki Ubunifu yaliyotolewa na BRELA kwa wanafunzi na wahadhiri wa Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA) wakiwa katika picha ya pamoja na watumishi wa Wakala baada ya mafunzo hayo ya siku moja (1) yaliyofanyika chuoni hapo jijini Dar es Salaam.*

Alisema TIA ikilinda vumbuzi hizo zitakuwa na manufaa kwa mbunifu, chuo na jamii kwa ujumla.

Alifafanua kuwa haki za Miliki Ubunifu, ikiwemo Hataza, Alama za Biashara na Huduma, zimekuwa na thamani ulimwenguni, hivyo bunifu wanazozianzisha au wanazobuni wahakikishe wanazisajili BRELA ili zilindwe na ziweze kunufaisha na kusaidia jamii.

Kwa upande wake, Msaidizi wa Usajili wa BRELA, Bw. Benedickson Byamanyilwowa, alisisitiza kuwa Hataza zinazobuniwa katika Miliki Ubunifu zote zinazosimamiwa na kulindwa na BRELA.

Alieleza kuwa usajili wake unafanyika kwa njia ya mtandao ambao unapatikana katika tovuti ya Taasisi ya www.brela.go.tz.

Taasisi imewarahisishia wadau lengo likiwa ni kuokoa muda na kupunguza gharama.

Awali, akitoa neno la ukaribisho, Mkuu wa Idara ya Ukuzaji na Uendelezaji wa Wanafunzi Kitaaluma na Kitaalam, Bw. Imani Matonya, aliipongeza BRELA kwa kuandaa mafunzo hayo ya Miliki Ubunifu na kufika katika chuo hicho ambacho kinafundisha taaluma mbalimbali ikiwemo ya Miliki Ubunifu na Elimu ya Biashara.

## Mawakili, wafanyabiashara ...

hiyo kutumia vyombo vyao kusaidia kufikisha elimu itakayotolewa kuhusu dhana ya Wamiliki Manufaa na kuhakikisha inawafikia wadau na wananchi wote.

Sambamba na warsha hiyo, BRELA iliandaa kliniki ya biashara (Business Clinic) ya siku tatu katika eneo la Stendi Kuu ya mabasi ili kutoa msaada wa usajili na elimu wezeshi kwa waliokuwa na uhitaji wa huduma hiyo.

Akiongea kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa huo, Bw. Mmbando aliwaomba wananchi wa jiji la Arusha na viunga vyake waweze kufika kujipatia huduma hizo muhimu.

# BRELA kupokea maoni ya uboreshaji wa sheria ya kampuni na majina ya biashara

**Na Christina Njovu**





*Washiriki wa kikao kazi cha kukusanya maoni ya wadau kuhusu maboresho ya Sheria ya Kampuni na Majina ya Biashara, wakisikiliza mada mbalimbali Machi,12, 2024 Jijini Dar es Salaam.*

Katibu Mkuu Wizara ya Viwanda na Biashara, Dkt. Hashil Twalibu Abdallah, amewataka washiriki wa kikao kazi cha kupitia Sheria ya Kampuni na Majina ya Biashara kuchangia mawazo yatakayosaidia Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania kufanya utafiti utakaoiwezesha serikali kuchukua hatua stahiki za kuboresha sheria hizo.

Kikao kiliandaliwa kwa lengo la kutoa nafasi kwa washiriki kupitia na kujadili kwa kina masuala mbalimbali muhimu kuhusu utekelezaji wa Sheria ya Kampuni, Sura 212 na Sheria ya Majina ya Biashara, Sura 213.

Dkt. Abdallah alitoa rai hiyo katika hotuba ya ufunguzi iliyosomwa kwa niaba yake na Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Ushindani, Bw. William Erio, Machi 12, 2024 katika kikao kazi cha siku mbili cha kukusanya maoni ya wadau kuhusu maboresho ya Sheria ya Kampuni na Majina ya Biashara kilichofanyika kwa siku mbili katika Ukumbi wa Kilimanjaro Millenium Towers Jijini Dar es Salaam.

"Na hii itaiwezesha Wizara ya Viwanda na Biashara yenye dhamana ya kusimamia masuala ya viwanda na biashara, kutoa fursa ya pekee itakayowezesha kuwa na sheria bora zinazoweka mazingira wezeshi ya kurahisisha uendeshaji wa biashara nchini," alisema Erio.

Aliwataka washiriki kuungana pamoja na kuendelea kuzingatia kanuni, taratibu na sheria zinazosimamia masuala ya uendeshaji wa biashara pamoja na kuendelea kutoa maoni ya maboresho ya utekelezaji wa sheria zinazosimamia masuala ya biashara nchini kwa lengo la kuunga mkono jitihada za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika kuhamasisha uwepo wa mazingira mazuri ya uwekezaji na uendeshaji wa biashara katika nchi, alisisitiza Bw. Erio

Kikao kazi hicho cha kukusanya maoni ya wadau kuhusu maboresho ya Sheria ya Kampuni na Majina ya Biashara kiliandaliwa na Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania na kuwashirikisha mawakili, wahasibu, Wizara ya Viwanda na Biashara na BRELA.

## Wahadhiri, wanafunzi ...

Aliitaka BRELA kuendelea kufika chuoni hapo inapopewa mialiko ili kuendelea kutoa mafunzo kuhusu huduma zinazotolewa na taasisi hiyo.

Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Masoko cha TIA, Bi. Lilian Rugaitika, aliishukuru BRELA kwa mafunzo ya Miliki Ubunifu kwa wanafunzi na watumishi kwa sababu chuo kikuu ni taasisi inayotoa elimu kwa nadharia na vitendo, hivyo ujio wa BRELA ulikamilisha dhana ya kutoa elimu kwa vitendo.



*Baadhi ya wahadhiri na wanafunzi kutoka Taasisi ya Uhasibu (TIA) Dar es Salaam wakisikiliza mawasilisho kutoka kwa watumishi wa BRELA kuhusu dhana ya Miliki Ubunifu wakati wa mafunzo yaliyotolewa na BRELA chuoni hapo*

# BRELA yatakiwa kuongeza kasi utoaji elimu

**Na Sheila Mfunami**

BRELA imetakiwa kuongeza kasi ya utoaji wa elimu kwa wafanyabiashara kuhusu huduma inazotoa, hasa matumizi ya Mifumo ya Usajili kwa njia ya Mtandao (ORS), ili kutatua changamoto zinazojitokeza kwa baadhi ya wafanyabiashara kushindwa kutumia mifumo hiyo.

Wito huo ulitolewa Januari 25, 2024 na Jaji Mfawidhi Divisheni ya Kazi, Dkt. Yose Mlyambina, alipotembelea banda la BRELA wakati wa maonesho yaliyoambatana na Maadhimisho ya Wiki ya Sheria katika viwanja vya Mnazi Mmoja, jijini Dar es Salaam.

Alisisitiza kwamba BRELA ni kiungo muhimu katika uanzishaji na uendeshaji wa biashara nchini, hivyo licha ya kazi kubwa inayofanya haina budi kuongeza kasi ya utoaji elimu ili wadau wafikiwe na wanufaike na uwepo wa taasisi hiyo.

Dkt. Mlyambina aliongeza kuwa kumekuwa na uelewa mdogo wa utumiaji wa mifumo ya BRELA na kusababisha baadhi ya maombi kutokamilika kwa wakati, hivyo ni muhimu kuongeza nguvu katika kutoa elimu.




*Afisa wa BRELA Bw. Ndeyanka Mbowe akimkabidhi cheti cha usajili wa Jina la Biashara mmoja wa wateja waliotembelea Banda la Wakala wakati wa Maadhimisho ya Wiki ya Sheria Januari 25, 2024 katika Viwanja vya Mnazi Mmoja, Dar es Salaam.*

“Mmekuwa watendaji wazuri sana kwenye upande wa utoaji wa huduma kwa njia ya mtandao, hivyo maadhimisho haya yawe chachu kwa wafanyabiashara na wadau kwa ujumla ya kurasimisha biashara zao na kutatua changamoto za kisheria,” alisema.

Aliwataka wadau mbalimbali kutembelea maonesho hayo katika banda la BRELA waweze kurasimisha biashara zao pamoja na kutatua changamoto mbalimbali kwani huduma zilikuwa zinatolewa papo kwa papo. Maonesho hayo yaliyoanza Januari 24, 2024 yalihitimishwa Januari 30, 2024.




*Jaji Mfawidhi Divisheni ya Kazi, Dkt. Yose Mlyambina, akiwa na Afisa wa BRELA alipotembelea banda la Taasisi wakati wa Maadhimisho ya Wiki ya Sheria Januari 25, 2024, katika Viwanja vya Mnazi Mmoja, Dar es Salaam.*

# Elimu ya dhana ya wamiliki manufaa yaendelea kutolewa

**Na Lugano Mwakyombe**

BRELA imeendelea kutoa elimu kwa taasisi za udhibiti mkoani Mwanza kuhusu dhana ya Miliki Manufaa lengo likiwa ni kuhamasisha na kuongeza kasi ya uwasilishaji wa taarifa za Wamiliki Manufaa kwa Msajili wa Kampuni.

Elimu hiyo ilitolewa wakati wa semina iliyofanyika Februari 5, 2024, katika ukumbi wa Hoteli ya Victoria Palace, jijini Mwanza.

Akizungumza kwa niaba ya Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, Afisa Sheria Mkuu, Bw. Meinrad Rweyemamu, alisema mbali na kuelimisha, pia watatumia fursa hiyo kutatua changamoto mbalimbali ambazo wadau wanakumbana nazo wakati wa kufanya sajili kupitia Mfumo wa Usajili kwa njia ya Mtandao (ORS).

"Kwa siku ya Februari 6, 2024 tunatarajia kuwa na mwendelezo wa semina ambapo wadau mbalimbali wataelimishwa kuhusu dhana nzima ya Miliki Manufaa na baada ya semina hiyo tunatarajia kuwa na *Business Clinic* (Kliniki ya Biashara) ya siku tatu katika viwanja vya Rock City Mall kuanzia tarehe 7 hadi 9 Februari, 2024, ambako huduma mbalimbali za papo kwa papo zitatolewa. Nipende kuwakaribisha wadau kuja kupata huduma zetu," alisema Bw. Rweyemamu.

Aliongeza kuwa wakiwa hapo pia watatoa usaidizi kwa wadau walioshindwa kuwasilisha taarifa za mwaka za kampuni pamoja na taarifa za Wamiliki Manufaa.

Kuhusu sheria zinazohusu dhana ya Miliki Manufaa, Afisa Usajili wa BRELA, Bw. Jacob Mkuye, alifafanua kuwa uwasilishaji wa taarifa za Wamiliki Manufaa wa Kampuni ni zoezi endelevu lililoanza tangu mwaka 2021 na lipo kisheria ambapo kampuni zinapaswa kuwasilisha taarifa za Wamiliki Manufaa wake kwa Msajili wa Kampuni.

Bw. Mkuye alieleza kuwa uwasilishaji wa taarifa unafanyika kwa usiri na si kila mtu anapaswa kufahamu taarifa za Wamiliki Manufaa katika kampuni husika.

Alisisitiza kuwa taarifa hizo haziwekwi wazi kutokana na unyeti wake. Hivyo alitoa wito kwa kampuni ambazo bado hazijawasilisha taarifa, kufanya hivyo kwa wakati, ili kuepuka faini ya ucheleweshaji wa kuwasilisha taarifa hizo kwa Msajili.

Naye Afisa Usajili wa BRELA, Bi. Gift Wazingwa, alielezea juu ya miongozo mbalimbali ya kimataifa kuhusu dhana ya Miliki Manufaa ambapo alisema kuwa mataifa mengi duniani yalianza kuwasilisha taarifa hizo kwa muda mrefu ikilinganishwa na Tanzania ambayo uwasilishaji wake ulianza mwaka 2021.

Aliongeza kuwa uwasilishaji wa taarifa hizo ni muhimu kwa sababu ni takwa la kisheria linalohitaji kampuni kuwasilisha taarifa za Wamiliki Manufaa wake kwa Msajili.



*Washiriki kutoka Taasisi za uchunguzi wakiwa katika picha ya pamoja na watumishi wa BRELA baada ya kuhudhuria semina ya siku moja kuhusu dhana ya wamiliki manufaa iliyofanyika Victoria Palace Februari 5, 2024, jijini Mwanza.*

# Watumishi BRELA wajengewa uwezo uendeshaji mashauri, uandishi wa maamuzi

**Na Lugano Mwakyombe**

Watumishi wa BRELA wamejengewa wa uendeshaji wa mashauri na uandishi wa maamuzi kuhusu Alama za Biashara na Huduma pamoja na usimamizi wa sheria mbalimbali zinazosimamiwa na taasisi hiyo.

Mafunzo hayo yalifanyika Januari 24 hadi 26, 2024, katika Ukumbi wa Mikutano wa Kituo cha Uhasibu (APC), Jijini Dar es Salaam.

Akifungua mafunzo hayo kwa niaba ya Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, Kaimu Mkurugenzi wa Miliki Ubunifu Bi. Loy Mhando alisema ili kuboresha utendaji kazi wa watumishi katika kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa sheria zinazosimamiwa na BRELA, maofisa wanajengewa uwezo kuhusu uchakataji, uendeshaji wa mashauri na uandishi wa maamuzi kupitia mafunzo yaliyoandaliwa na Taasisi kuhusu masuala hayo.

Mafunzo hayo yalitolewa na Majaji wastaafu wa Mahakama Kuu ya Tanzania --. Prof. Robert Makaramba, Dkt. Fauz Twaib na John Mgetta.

Akiwasilisha mada kuhusu utendaji wa BRELA ikiwa ni ofisi inayosimamia sheria mbalimbali za usajili na utoaji leseni za biashara, Prof. Makaramba alisema maofisa wanapaswa kuendelea kutekeleza wajibu wao katika kusimamia na kufanyia kazi maombi yanayowasilishwa chini ya sheria zinazosimamiwa na Taasisi hiyo.

Aliwataka maofisa hao kuongeza umakini katika uchakataji wa maombi, uendeshaji wa mashauri pamoja na uandishi wa maamuzi ya maombi na mashauri ya Alama za Biashara na Huduma yanayowasilishwa BRELA kwa ajili ya kusikilizwa na kutolewa maamuzi.

Kwa upande wake, Jaji mstaafu Mgetta aliwasilisha mada ya utaratibu wa kupinga maombi ya usajili wa Alama za Biashara na Huduma pamoja na mada kuhusu uzingatiaji wa maadili katika mchakato mzima wa kuendesha mashauri.

Aliwataka watumishi kuwa makini na kujiepusha na vitendo vinavyokiuka maadili katika uendeshaji wa mashauri na uandaaji wa maamuzi ya mashauri hayo yanayofanyika kupitia sheria zinazosimamiwa na BRELA.



*Washiriki wa mafunzo ya BRELA kuhusu uendeshaji wa mashauri ya Alama za Biashara na Huduma wakifuatilia kwa makini mawasilisho yaliyotolewa na Jaji Mstaafu Prof. Robert Makaramba (hayupo pichani) Januari 25, 2024 katika Ukumbi wa Mikutano wa Kituo cha Uhasibu (APC), Jijini Dar es Salaam.*

" Aliwataka watumishi kuwa makini na kujiepusha na vitendo vinavyokiuka maadili

Naye Jaji Mstaafu Dkt. Twaib alisisitiza juu ya taratibu bora za uandishi pamoja na kuzingatia kanuni za uendeshaji wa mashauri katika lugha nyepesi ili kurahisisha uelewa kwa wahusika wa mashauri hayo.

Aliwakumbusha washiriki kuwa kesi zinazoendeshwa pamoja na maamuzi yanayotolewa siyo ya Msajili bali ni ya pande zinazohusika katika mashauri hayo, hivyo ni lazima yawe katika lugha rahisi inayoeleweka kwa wahusika wote katika kesi husika.




*Washiriki wa mafunzo ya BRELA wakiwa katika picha ya pamoja na wakufunzi walioketi kutoka kulia ni Kaimu Mkurugenzi wa Miliki Ubunifu Bi. Loy Mhando, Jaji Mstaafu John Mgetta, Prof. Robert Makaramba (katikati), Dkt. Fauz Twaib na Afisa Usajili Mwandamizi Bw. Seka Kasera (wa mwisho kushoto) baada ya kuhitimisha mafunzo Januari 26, 2024 katika Kituo cha Uhasibu, Bunju, jijini Dar es Salaam.*

# Punguzeni kero kwa wafanyabiashara - Serukamba

**Na Christina Njovu**

Maafisa biashara nchini, wametakiwa kutoa elimu kwa wananchi sambamba na kupunguza kero mbalimbali, zikiwemo gharama zisizo halali za urasimishaji biashara, suala ambalo serikali imekuwa ikilipigia kelele kwa nguvu zote mara kwa mara.

Aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Selukamba, alitoa wito huo Januari 9, 2024, wakati akifungua mafunzo ya kuwajengea uwezo maafisa biashara kutoka mikoa ya Dodoma, Singida, Rukwa, Simiyu, Katavi na Tanga yaliyofanyika mkoani Singida.

"Mafunzo haya ni muhimu, ukizingatia kwamba hivi sasa masuala ya uboreshaji wa mazingira ya biashara na uwekezaji, ikiwemo utoaji wa huduma za leseni za biashara na viwanda, hufanyika kwa njia ya mtandao kupitia mifumo ya kielektroniki au mifumo ya TEHAMA." Alisema.

Alisema kuwa ni matumaini yake kwamba mafunzo hayo ni chachu kwa maafisa biashara kwa sababu yatawawezesha siyo tu katika kutoa elimu kwa wananchi pia kuwa ni nyenzo ya kupunguza kero mbalimbali zikiwemo gharama za urasimishaji biashara, suala ambalo Serikali imekuwa ikilipigia kelele mara kwa mara kwa nguvu zote.

Alisisitiza kuwa mpango huo wa mafunzo umezingatia umuhimu wa maafisa biashara kuwa karibu na wananchi, kwa kutoa huduma bora, saidizi na elimishi kwao ili kipato chao kikue na hatimaye serikali iongeze mapato na uchumi wa nchi uweze kuimarika.

Awali Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, Bw. Godfrey Nyaisa, akimkaribisha Mkuu wa Mkoa huyo kufungua mafunzo hayo alieleza kuwa, maafisa biashara wanatakiwa kubadilisha mtazamo na kutambua majukumu ya Idara yao kwa kuachana na mtazamo wa kufunga biashara.

Aliwataka kuwatambua wafanyabiashara katika maeneo yao na kusikiliza kero zao zinazosababisha kufunga biashara ili biashara hizo ziendelee.

Pia aliwataka kutambua malengo ya idara yao ambayo ni mpya na majukumu yake ni pamoja na kubaini fursa za uwekezaji na kuweka mazingira wezeshi yatakayosaidia kukuza biashara na kuinua uchumi wa Halmashari na mkoa husika kwa ujumla.

"Kama mnavyofahamu, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan imedhamiria kuboresha na kuimarisha mazingira ya biashara nchini ili kuendana na azma ya kufanya mageuzi ya kiuchumi na viwanda kwa ajili ya kuleta maendeleo endelevu ya jamii,



*Baadhi ya washiriki wa mafunzo kwa Maafisa Biashara kutoka mikoa ya Singida, Dodoma, Simiyu, Katavi na Tanga wakimsikiliza aliyekuwa Mkuu wa Mkoa Singida, Peter Serukamba, Januari 9, 2024, akifungua mafunzo hayo ya siku nne yaliyofanyika mkoani Singida.*

kama ilivyoainishwa katika Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025 na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano," alifafanua Bw. Nyaisa.

Mafunzo hayo yaliandaliwa na BRELA kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Wizara ya Viwanda na Biashara kwa lengo la kuwajengea uwezo maafisa biashara nchini.





*Washiriki wa mafunzo ya maafisa biashara wakiwa katika picha ya pamoja na aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, (katika) na Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA Bw. Godfrey Nyaisa (kulia) baada ya ufunguzi wa mafunzo Januari 9, 2024 mkoani Singida.*

# Maafisa biashara watakiwa kuleta mabadiliko idara mpya ya viwanda, uwekezaji

**Na Christina Njovu**

Maafisa biashara wametakiwa kutumia elimu waliyoipata kubadilisha mtazamo wao na kutekeleza majukumu ya idara mpya ya Biashara Viwanda na Uwekezaji kwa ufanisi.

Wito huo ulitolewa Januari 12, 2024, na Mkurugenzi wa Leseni wa BRELA, Bw. Andrew Mkapa, wakati akifunga mafunzo ya siku nne wa maafisa biashara kuhusu Sheria ya Leseni za Biashara na Viwanda yaliyofanyika mkoani Singida.

"Ndugu washiriki, mafunzo haya yasiishie hapa, tuendelee kuwasiliana hata tukirudi katika maeneo yetu ya kazi, tushauriane pale inapohitajika na tubadilishane uzoefu juu ya jambo lolote," alisema Bw. Mkapa

Akitoa ushauri kwa maafisa biashara hao, Bw. Mkapa alieleza kuwa baada ya mafunzo hayo anategemea kutakuwa na mabadiliko katika utendaji kazi na busara ikitawala zaidi katika kuwasilisha namna ya kuleta mabadiliko hayo katika utekelezaji wa majukumu.

Akitoa shukrani kwa niaba ya washiriki wengine, Afisa Biashara wa Manispaa ya Mpanda, Bw. Paul Kahoya, aliahidi kwenda kuyatekeleza yote waliyojifunza sambamba na kuzisoma sheria ambazo zitakuwa mwongozo katika kutekeleza majukumu yao.

BRELA
BUSINESS REGISTRATIONS AND LICENSING AGENCY



FAHAMU KUHUSU MFUMO WA KUWASILISHA TAARIFA ZA WAMILIKI MANUFAA

Mfumo wa kupokea taarifa za Wamiliki Wanufaika ni mfumo unaojitegemea kutoka kwenye mfumo wa **Online Registration System (ORS)** hivyo kampuni ambazo zina maombi yanayoendelea kwenye ORS bado zinaweza kuwasilisha taarifa zake za Wamiliki Manufaa kupitia link ya **https://bo.brela.go.tz**

"TUNAIPA UHAI WA KISHERIA BIASHARA YAKO"

# Huduma za BRELA zawafikia walemavu Kondoa



*Baadhi ya washiriki wa mafunzo ya siku moja kuhusu huduma za BRELA yaliyotolewa kwa wenye ulemavu wa kusikia yaliyofanyika tarehe 6 Februari, 2024 wilayani Kondoa*

## Maafisa biashara watakiwa kuleta ...

Aliongeza kuwa yote waliyojifunza ni nyenzo muhimu katika kutekeleza majukumu yao ambapo kwa sasa wamepewa idara. Alisisitiza kuwa anaamini kwamba uanzishwaji wa idara ya Biashara, Viwanda na Uwekezaji chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara itawawezesha kutekeleza majukumu yao ipasavyo. Aliendelea kwa kusema kuwa ni wazi kwamba Serikali imeona kuna tija, hivyo watafanya kazi kwa weledi kwa kuzingatia sheria na miongozo waliyopewa.

Mafunzo hayo yaliandaliwa na BRELA kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) pamoja na Wizara ya Viwanda na Biashara kwa lengo la kuwajengea uwezo Maafisa Biashara ili waweze kufanya kazi kwa ufanisi zaidi. Mafunzo haya yalihudhuriwa na washiriki ambao ni Maafisa Biashara kutoka mikoa ya Singida, Dodoma, Rukwa, Simiyu, Katavi na Tanga.



*Maafisa Biashara wakishiriki mafunzo ya kuwajengea uwezo yaliyoandaliwa na BRELA*

**Na Njwaba Mwaijibe**

BRELA imetoa elimu kuhusu huduma zake kwa watu wenye ulemavu wa kusikia (viziwi) katika Wilaya ya Kondoa, mkoani Dodoma.

Elimu hiyo ilitolewa Februari 6, 2024, kwa lengo la kuhamasisha kundi hilo maalum ili kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu huduma zinazotolewa na BRELA.

Akizungumza katika mafunzo hayo, Afisa Leseni, Bi. Winfrida Gaudence, alisema kuwa Taasisi imeitikia ombi la Taasisi ya Maendeleo ya Viziwi Tanzania (TAMAVITA) la kuwapatia elimu hiyo ambayo ni yenye manufaa kwa biashara zao.

Alieleza kuwa faida za kurasimisha biashara BRELA ni pamoja na kuwa na upekee katika soko, kunufaika pale wanapohitaji mikopo katika taasisi za fedha, kupata fursa mbalimbali ikiwa ni pamoja na fursa za ukuzaji wa biashara.

"Niwapongeze kwa mwitikio wenu na tumefurahi kujumuika nanyi Ili kuwapatia elimu hii ya urasimishaji wa biashara na ninaamini mtakwenda kuitumia vema na kwa kuwa tumefika hapa, kwa wale wenye uhitaji wa usaidizi katika Mfumo wa Usajili kwa njia ya Mtandao (ORS), tupo kufanikisha hilo," aliongeza Bi. Gaudence.

Sambamba na hilo, aliwaomba wenye vikundi vya kibiashara kusajili majina yao au kampuni na kupata leseni ili iwe rahisi kufanya biashara kwa uhuru zaidi.

Kwa upande wake Mtendaji Mkuu wa TAMAVITA, Bw. Kelvin Nyema, aliipongeza BRELA kwa kufika wilayani Kondoa na kukutana na watu wenye ulemavu wa kusikia na kuwapatia elimu ambayo itawasaidia kujikwamua na kusonga mbele zaidi kwenye biashara zao.

"Naomba kwanza mfikishie salamu Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA kuwa tunashukuru sana kwa kufadhili na kufanikisha

# Huduma za BRELA zawafikia ...

mafunzo haya, niwahikikishie watu wenye ulemavu wa kusikia kuwa elimu waliyoipata leo itafungua fursa zaidi kwani kuna wafanyabiashara, wakulima na hata wajasiriamali ambao waliihitaji sana elimu hii," aliongeza Bw. Nyema.

Mafunzo hayo ya siku moja yaliyofadhiliwa na BRELA na kuwakutanisha viziwi wapatao 50 ambao kwa umoja wao walisema wamehamasika na kuwa watakuwa mabalozi wa huduma za BRELA.



*Mtumishi wa BRELA Bi. Winfrida Gaudence akiwasilisha mada kwa washiriki wa mafunzo yaliyoandaliwa na Wakala kwa kushirikiana na CHAMAVITA kwa watu wenye ulemavu wa kusikia yaliyofanyika Februari 6, 2024 wilayani Kondoa*





# Taasisi za Uchunguzi zanolewa kuhusu dhana ya Umiliki Manufaa

**Na Christine Njovu**

BRELA imetoa mafunzo kuhusu namna ya kutambua mmiliki manufaa wa Kampuni na Majina ya Biashara kwa taasisi za uchunguzi ili kurahisisha utekelezaji wa majukumu yao ya kuzuia na kupambana na uhalifu wa kifedha.

Mafunzo hayo yalifanyika Jijini Arusha Februari 26, 2024.

Kaimu Mkurugenzi wa Kampuni na Majina ya Biashara BRELA, Bw. Isdor Nkindi, alieleza kuwa Wakala imekasimiwa na serikali pendekezo namba 24 kati ya mapendekezo 40 ya kikosi kazi cha kushughulika na makosa ya uhalifu wa kifedha ulimwenguni (FATIF) linalohimiza uwazi katika kampuni.

"kutokana na jukumu hilo kila nchi mshirika inawajibika kuwajengea uwezo na miundombinu kwa ajili ya kukabiliana na makosa kama hayo, hivyo ni muhimu kukutana na taasisi zinazo shughulika na uhalifu ili tuweze kuzungumza lugha moja, pale ambapo uhalifu unatokea na hata kabla ya kutokea uweze kudhibitiwa," alisema Bw. Nkindi.

Alitoa wito kwa kila taasisi iweze kutimiza wajibu wake, BRELA ikishakamilisha kufanya sajili, taasisi kama TAKUKURU na Polisi waende kuchukua taarifa hizo pindi viashiria vya uhalifu vinapojitokeza ili kuzuia uhalifu usiweze kutokea.

Katika mafunzo hayo Nkindi alizitaka taasisi hizo kufuata utaratibu wa kuomba taarifa kupitia mamlaka zao badala ya mtumishi mmoja mmoja kuomba pekee yake.

Mafunzo hayo yaliyofanyika kwa siku moja yalihudhuriwa na taasisi zipatazo kumi, zikiwemo Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Polisi, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Uhamiaji, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na Mahakama ya Tanzania.



*Mkurugenzi wa Kampuni na Majina ya Biashara wa BRELA, Bw. Isdori Nkindi, akiwasilisha mada wakati wa mafunzo kwa Taasisi za Uchunguzi kuhusu namna ya kutambua Mmiliki Manufaa wa Kampuni na Majina ya Biashara Jijini Arusha.*

# Wanafunzi chuo kikuu cha kiislam Morogoro (MUM) waelimishwa urasimishaji wa biashara

**Na. Njwaba Mwaijibe**

Wanafunzi wa Chuo kikuu Cha Kiislam Morogoro (MUM), wamepewa elimu juu ya huduma zinazotolewa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) ili kuwa na uelewa juu ya huduma zinazotolewa na umuhimu wake.

Wanafunzi hao walipata elimu hiyo Desemba 13, 2023 walipofanya ziara ya mafunzo katika Ofisi za BRELA jijini Dar es Salaam.

Akiwalisha mada juu ya huduma zinazotolewa na Taasisi hiyo kwa wanafuzi hao, Afisa kutoka Kurugenzi ya Kampuni na Majina ya Biashara, Bi. Maryglory Mmari alisema kuwa, huduma zinatolewa na BRELA ni pamoja na Usajili wa Majina ya Biashara, Usajili wa Kampuni, Usajili wa Alama za Biashara na Huduma, Utoaji wa Leseni za Biashara kundi "A", Utoaji wa Leseni za Viwanda na Utoaji wa Hataza.

Aidha, Bi. Mmari alieleza kuwa sajili mbalimbali za BRELA ni muhimu kwa wadau kuzizingatia kwa sababu huwezesha biashara kutambulika na mamlaka mbalimbali ikiwa ni pamoja na kupata dhamana ya kukopesheka katika taasisi za kifedha.

"Mkumbuke kuwa mfanyabiashara anaporasimisha biashara yake anakuwa na wigo mpana katika soko sambamba na kupata nafasi ya kushinda zabuni mbalimbali ambazo hushindanishwa," alifafanua Bi. Mmari

Aliongeza kuwa mfanyabiashara aliyesajili biashara yake ana haki ya kipekee kutumia, Jina la Biashara, Kampuni, Leseni au Alama iliyosajiliwa na kuwa na haki ya kuwashitaki watakaotumia bila ridhaa yake.

Kwa upande wake Afisa kutoka Kurugenzi ya Leseni, Bw. Paul Peter aliwaeleza wanafunzi hao kuwa mfanyabiashara yeyote anatakiwa kukata Leseni kwani ndiyo kibali kitakachomuwezesha kufanya biashara husika, hivyo wale wenye biashara yenye sura ya kitaifa na kimataifa wanatakiwa kuwa na Leseni ya Biashara Kundi "A" ambayo hutolewa na BRELA.

Akizungumza kuhusu Miliki Ubunifu Bw. Benedickson Byamanyilwowa, alisema kuwa kwakuwa Miliki Ubunifu ni zao la akili ni vyema wavumbuzi wakajua umuhimu wa kulinda vumbuzi zao kwani ni bidhaa zenye thamani.

Aliongeza kwa kusema kuwa Alama ya Biashara au Huduma na Uvumbuzi uliosajiliwa BRELA, unamuwezesha mmiliki kuingia ubia wa kibiashara na wadau wengine na kujipatia faida.

Wanafunzi hao pia walielezwa kuhusu mahitaji na hatua za usajili zinazohitajika katika kukamilisha Usajili kupitia Mfumo wa Usajili kwa njia ya Mtandao (ORS).

Ziara ya wanafunzi hao katika Ofisi za BRELA ni mwendelezo wa Taasisi kutoa elimu kwa wadau mbalimbali kuhusu huduma zinazotolewa na BRELA ili kukuza uelewa wa wananchi.



*Wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Kiislam Morogoro (MUM) wakiwa katika picha ya pamoja na maafisa wa BRELA waliowasilisha mada kuhusu huduma zitolewazo na Wakala walipofanya ziara ya mafunzo tarehe 13 Desemba, 2023 katika Ofisi za BRELA jijini Dar es Salaam.*

# Zipeni ulinzi alama za biashara zenu – Kijaji

**Na Christine Njovu**

Waziri wa Viwanda na Biashara, Dkt. Ashatu Kijaji, amewataka wajasiriamali wanawake wanaoendesha biashara zao sokoni kurasimisha biashara zao na kuzisajili BRELA.

Alisema sajili ya alama za biashara zao itaongeza thamani na kulinda bunifu zao na kuwawezesha kunufaika nazo kiuchumi.

Dkt. Kijaji alitoa rai hiyo katika hotuba iliyosomwa kwa niaba yake na Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, Bw. Godfrey Nyaisa, Machi 7, 2024 ikiwa ni Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani yaliyoandaliwa na Wanawake wa Masokoni wa Mkoa wa Dar es Salaam (WOMEN TAPO) yaliyofanyika katika Viwanja vya Mnazi Mmoja, Jijini Dar es Salaam.

Katika hafla hiyo, Bw. Nyaisa aliwataka wanawake wajasiriamali kuacha kuendesha biashara kienyeji na kuwaeleza faida watakazopata kwa kusajili biashara na vumbuzi zao itakayowawezesha kupata fursa mbalimbali za kibiashara na ulinzi wa kisheria.

"Niwahakikishie kuwa BRELA inazipa ulinzi wa kisheria biashara na bunifu iwapo mtu yeyote ataiga kazi yako, kwa wewe mwanamke mjasiriamali uliye na usajili wa BRELA una haki ya kushtaki mahakamani na Wakala itasimama kukutetea kuwa hiyo ni mali yako" ameeleza Bw. Nyaisa

Alisisitizia kuongeza thamani bidhaa zao wanazozalisha kwa kuweka alama ya biashara kwenye bidhaa zao wanazozizalisha ili kutambulika kwa uharaka katika masoko na kuweza kuzitofautisha na bidhaa zingine.

Aliongeza kuwa mbali ya kupata ulinzi wa kisheria pia watapata fursa ya kukopesheka katika Taasisi rasmi za Kifedha ambako moja ya masharti lazima uwe umesajili biashara yako BRELA badala ya kuchukua mikopo umiza.

# BRELA yatinga Kilimanjaro International Marathon

**Na Tawi Kilumile**

Kwa mara ya kwanza Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) imeshiriki katika mashindano ya Kimataifa ya riadha masafa marefu maarufu kama Kili Marathon yaliyofanyika Februari 2024 mkoani Kilimanjaro. Mbio hizi hufanyika mwishoni wa mwezi Februari kila mwaka ili kutoa fursa kwa washiriki kupanda Mlima kama sehemu ya utalii.

Aidha, mashindano haya yaliyoanza mwaka 2002 yanalenga katika kuvutia watalii wa ndani na nje ya nchi kuja Tanzania katika Safu za Milima ya Kilimanjaro huku wakifurahia vivutio vilivyopo katika viunga vya Mkoa wa Kilimanjaro. Mashindano hayo yanahusisha mbio za urefu wa Kilomita 42.2 (Marathon), KM 21.1 (Half Marathon) na KM 5 (Fun run).

Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, Bw. Godfrey Nyaisa aliwaongoza watumishi watano (5) walioshiriki mashindano hayo ambayo yalihudhuriwa na wanamichezo watalii zaidi ya 12,000 kutoka pande zote za dunia. Aidha, Bw. Nyaisa alishiriki kwenye kundi la kilomita 21.1 ambapo alifanikiwa kumaliza na kukabidhiwa medali. Watumishi wengine ni pamoja na Bw. Tawi Kilumile, Bw. Tulizo Mpina, Bw. Onesmo Mushi na Bi. Gift Wazingwa.

Ushiriki wa BRELA katika mbio hizo ni sehemu kuunga mkono juhudi za Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kuhamasisha utalii, kujenga utamaduni wa watumishi wake kushiriki michezo mahali pa kazi ili kuimarisha afya za watumishi pamoja na kuimarisha ushirikiano wa BRELA na wadau wake. Pia unachangia kuitangaza Taasisi na huduma zake ambazo hutolewa kwa njia ya mtandao na kumwezesha Mteja kupata huduma hiyo popote alipo bila kulazimika kufika ofisi za BRELA.




*Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, Bw. Godfrey Nyaisa, akiongoza watumishi walioshiriki kwenye mashindano ya mbio za KiliMarathon Februari 25, 2024, mkoani Kilimanjaro.*

# Diamond aibukia BRELA kupata elimu ya urasimishaji biashara

**Theresa Chilambo**

Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, Bw. Godfrey Nyaisa, Machi 7, 2024, alikutana na kufanya mazungumzo na mwanamuziki wa kizazi kipya na Mkurugenzi wa Wasafi Media, Bw. Naseeb Abdul, maarufu kwa jina la Diamond Platnumz, alipotembelea katika Ofisi za BRELA jijini Dar es Salaam.

Bw. Abdul alisema mbali na kuwa mwanamuziki yeye ni mfanyabiashara na mwekezaji ambaye hutengeneza na kuanzisha chapa na kuwainua vijana ili kujipatia kipato hivyo kama mfanyabiashara BRELA ni kama nyumbani.

“Nilipokutana na Bw. Godfrey Nyaisa na kujitambulisha kwangu alinieleza kuwa BRELA panafaa kuwa nyumbani kwako kwa sababu una chapa tofauti tofauti hivyo patakusaidia katika kusajili kazi zako ili usipoteze haki. Maneno hayo yalikuwa na maana kubwa katika maisha yangu na hapo ndipo nilipobadilisha mtazamo na kugundua vijana wengi wanapoteza haki zao,” alieleza Bw. Abdul.

Alisema wasanii, wanamichezo, vijana na yeyote mwenye lengo la kufika mbali kimaendeleo, hawezi kwenda mbele kama hajarasimisha biashara yake BRELA. Na ili kuwa rasmi unahitaji kusajili jina la biashara, kusajili kampuni na kufuata taratibu mbalimbali ambazo serikali wameweka kama njia nzuri ambazo zitalinda na kuwezesha kufika mbali.

Alisisitiza kuwa ni vyema kujitahidi kujirasimisha na kulinda alama ya biashara na huduma pamoja na vumbuzi BRELA ili kulinda ndoto yako kwasababu ukianzisha jambo na likawa kubwa ukigundua kuna mtu anatumia alama yako, kama yeye amewahi ameisajili kisheria ana uwezo wa kukupeleka katika vyombo vya sheria.




*Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, Bw. Godfrey Nyaisa alipokutana na kufanya mazungumzo na Mwanamuziki wa kizazi kipya na Mkurugenzi wa Wasafi Media, Bw. Naseeb Abdul maarufu kwa jina la Diamond Platnumz alipotembelea katika Ofisi za BRELA jijini Dar es Salaam.*

“Kwa watu ambao wanatumia *brand*s zetu pasipo kuwa na haki halali naelewa kibinadamu atakuwa anatafuta riziki lakini nawashauri waache na wasinilaumu baadae kwa sababu sheria itafuata mkondo wake hasa kwa kipindi hiki tumeamua kuwa makini zaidi katika biashara” alisisitiza Bw. Abdul.

Alihitimisha kwamba amegundua umuhimu wa sajili na amefanikiwa kuchukua hatua ya kulinda haki zake BRELA baada ya kufahamu kwa kina faida zake hivyo kuepuka hasara kubwa ambayo angeipata na kupelekea kupoteza pato la Taifa.



*Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, Bw. Godfrey Nyaisa akimkabidhi zawadi ya shajara ya BRELA mwanamuziki wa kizazi kipya na Mkurugenzi wa Wasafi Media, Bw. Naseeb Abdul maarufu kwa jina la Diamond Platnumz alipotembelea katika Ofisi za BRELA jijini Dar es Salaam.*

# Wafanyabiashara wakumbushwa dhana ya wamiliki manufaa

**Na Njwaba Mwaijibe**

Katika jitihada za kuendeleza sekta ya biashara nchini, BRELA imeendesha semina maalum kwa wadau wa biashara kuwaelimisha kuhusu dhana ya Wamiliki Manufaa iliyofanyika Februari 20, 2024 katika ukumbi wa Royal Tughimbe Hotel jijini Mbeya.

Akifungua semina hiyo kwa niaba ya Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, Mkurugenzi wa Kampuni na Majina ya Biashara, Bw. Isdori Nkindi, alisema mwaka huu BRELA imejikita katika kuangazia changamoto zinazojitokeza wakati wa kufanya usajili ili kuona namna gani wanaweza kuepukana na vitendo hatarishi hii ni kutokana na baadhi ya kampuni nchini kutumika vibaya kwa kufanya vitendo vya uhalifu ikiwa ni pamoja na utakatishaji wa fedha haramu, kufadhili vitendo vya ugaidi na ukwepaji wa kodi.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti katika semina hiyo, washiriki wa mafunzo hayo waliipongeza BRELA kwa kuandaa mafunzo hayo yaliyowaleta pamoja wadau wa sekta ya biashara jijini Mbeya kujadili namna ya kuongeza mchango katika maendeleo ya biashara hususan katika kukuza uchumi nchini.



*Watumishi wa BRELA Bi. Upendo Maeda na Bi. Vicensia Fuko wakitoa elimu kwa mfanyabiashara jijini Mbeya wakati wa zoezi la ukaguzi elimishi Februari, 2024*

Mmoja wa wafanyabiashara hao, Bw. Tumaini Yolim, alisema ni muhimu kuwepo kwa ushirikiano wa karibu kati ya BRELA na wafanyabiashara ili kuchochea ukuaji wa uchumi jumuishi utakaowezesha kutatua changamoto za wafanyabiashara kwa wakati.

Mmiliki wa Kampuni ya Mghaka, Bw. Peter Wegesa Chacha, alisema BRELA iwe mstari wa mbele katika kuwasaidia wafanyabiashara wadogo kuweza kusajili biashara zao kwa kuwa baadhi yao wamekuwa waoga kurasimisha biashara zao. Hii ni kutokana na uelewa mdogo wa kufahamu umuhimu huo.

Mbali na utoaji mafunzo, BRELA pia ilitoa huduma za papo kwa papo kwa wafanyabiashara kuanzia Februrai 21 hadi 23, 2024 katika viwanja vya Kabwe jijini Mbeya.



*Watumishi wa BRELA wakihojiana na wafanyabiashara jijini Mbeya wakati wa zoezi la ukaguzi elimishi, Februari, 2024*

BRELA

Pata taarifa zaidi kuhusu huduma zetu, na jihudumie mwenyewe kupitia link ya **https://ors.brela.go.tz**





*Baadhi ya watumishi wa BRELA wakijiandaa kwa mazoezi Machi, 2024 katika uwanja wa mpira wa Shule ya Msingi Zanaki jijini Dar es Salaam.*



*Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, Bw. Godfrey Nyaisa, na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Biashara Tanzania (TCB), Bw. Adam Mihayo, (kushoto), wakiwa katika picha ya pamoja na watumishi wa BRELA na TCB mara baada ya majadiliano kuhusu ushirikiano katika utoaji huduma kwa wadau baina ya taasisi hizo mbili yaliyofanyika Machi 5, 2024 katika ofisi za BRELA jijini Dar es Salaam*



*Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, Bw. Godfrey Nyaisa, (kulia) akiwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Biashara Tanzania (TCB), Bw. Adam Mihayo, (kushoto) mara baada ya majadiliano kuhusu ushirikiano katika utoaji huduma kwa wadau baina ya taasisi hizo mbili yaliyofanyika Machi 5, 2024 katika ofisi za BRELA jijini Dar es Salaam.*



*BRELA yakabidhiwa cheti cha utambuzi kama mdau kutokana na mchango inaotoa katika kufanikisha huduma za kiforodha nchini na Umoja wa Forodha Duniani (WCO). BRELA ilikabidhiwa cheti hicho na kupokelewa na Bi. Theressa Chilambo, (kulia), kwa niaba ya Afisa Mtendani Mkuu, wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Forodha Duniani Januari 26, 2024 jijini Dar es Salaam.*



*Afisa wa BRELA Bw. Yusufu Mwasakafyuka akitoa mada kuhusu huduma za Taasisi kwa wananfunzi wa Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM) walipofanya ziara ya mafunzo Januari 19, 2024 katika ofisi za BRELA jijini Dar es Salaam.*






**Kushoto:** *Watumishi wa BRELA wakimsikiliza mteja aliyefika kupata elimu kuhusu utaratibu wa usajili kupitia mfumo kwa njia ya mtandao – ORS wakati wa Maadhimisho ya Wiki ya Sheria yaliyofanyika katika viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam, Januari 25, 2024.* ***Kulia:*** *Afisa wa BRELA akitoa huduma saidizi kwa wateja waliofika kufanya usajili wa majina ya biashara katika viwanja vya Mnazi Mmoja wakati wa Wiki ya Sheria.*






***Picha kushoto:*** *Mkurugenzi wa Leseni wa BRELA, Bw. Andrew Mkapa, akisaini kitabu cha wageni kwenye mmoja ya mabanda ya wadau walishiriki Maadhimisho ya Wiki ya Sheria, Viwanja vya Nyerere Square jijini Dodoma.*

***Picha kulia:*** *Baadhi ya wateja waliofika kupata huduma katika banda la BRELA wakiwa na Cheti cha usajili baada ya kukalisha usajil wa jina la biashara wakati wa Maadhimisho ya Wiki ya Sheria kwenye viwanja vya Nyerere Square jijini Dodoma Januari, 2024.*



*Jaji Mfawidhi Divisheni ya Kazi, Dkt. Yose Mlyambina, akisaini kitabu cha wageni alipotembelea banda la BRELA wakati wa Maonesho ya Maadhimisho ya Wiki ya Sheria yaliyofanyika katika viwanja vya Mnazi mmoja, jijini Dar es Salaam, Januari 25, 2024.*




*Watumishi wa BRELA wakiwa katika picha ya pamoja na wawezeshaji wa mafunzo kuhusu uendeshaji wa mashauri ya alama za biashara na huduma yaliyofanyika Ukumbi wa Mikutano wa Kituo cha Uhasibu, Bunju, Dar es Salaam Januari 25, 2024*





*Baadhi ya wanafunzi kutoka Chuo cha Usimamizi wa Fedha walipofika ofisi za BRELA jijini Dar es Salaam Januari,19, 2024 kujifunza majukumu ya Taasisi*






*Wadau wakiendeea kupata huduma mbalimbali katika maadhimisho ya wiki ya sheria, katika viwanja vya Nyerere Square, Dodoma, mwezi Januari 2024.*



*Watumishi wa BRELA, Bi. Winfrida Gaudence na Farid Hoza, wakiwa wameshika cheti cha ushiriki katika Maonesho ya Wiki ya Sheria yaliyohitimishwa Januari 30, 2024 katika Viwanja vya Nyerere Square, Jijini Dodoma. BRELA ilishiriki kwa kutoa huduma za papo kwa papo za urasimishaji biashara na kutoa usaidizi kwa wadau juu ya matumizi ya Mfumo wa Usajili wa njia ya Mtandao (ORS).*



*Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, Bw. Godfrey Nyaisa, (kulia) akiwa katika picha ya pamoja na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Biashara Tanzania (TCB), Bw. Adam Mihayo, (kushoto), mara baada ya majadiliano kuhusu jinsi ya kuimarisha ushirikiano katika utoaji huduma kwa wadau baina ya Taasisi hizi mbili Machi 5, 2024 katika ofisi za BRELA jijini Dar es Salaam.*



*Watumishi wa BRELA, Bi. Winfrida Gaudence na Farid Hoza, wakiwa wameshika cheti cha ushiriki katika Maonesho ya Wiki ya Sheria yaliyohitimishwa Januari 30, 2024 katika Viwanja vya Nyerere Square, Jijini Dodoma. BRELA ilishiriki kwa kutoa huduma za papo kwa papo za urasimishaji biashara na kutoa usaidizi kwa wadau juu ya matumizi ya Mfumo wa Usajili wa njia ya Mtandao (ORS).*



*Mkurugenzi wa Leseni, Bw. Andrew Mkapa (kulia) akipokea mfuko toka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Biashara Tanzania (TCB), Bw. Adam Mihayo, (kushoto), mara baada ya majadiliano kuhusu jinsi ya kuimarisha ushirikiano katika utoaji huduma kwa wadau baina ya Taasisi hizi mbili Machi 5, 2024 katika ofisi za BRELA jijini Dar es Salaam.*



*Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, Bw. Godfrey Nyaisa, (kulia) akiwa katika picha ya pamoja na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Biashara Tanzania (TCB), Bw. Adam Mihayo, (kushoto), mara baada ya majadiliano kuhusu jinsi ya kuimarisha ushirikiano katika utoaji huduma kwa wadau baina ya Taasisi hizi mbili Machi 5, 2024 katika ofisi za BRELA jijini Dar es Salaam.*



*Kaimu Mhasibu Mkuu wa BRELA, Bi, Fatuma Mwenkale (kulia) akipokea mfuko kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Biashara Tanzania (TCB), Bw. Adam Mihayo, (kushoto), mara baada ya majadiliano kuhusu jinsi ya kuimarisha ushirikiano katika utoaji huduma kwa wadau baina ya Taasisi hizi mbili Machi 5, 2024 katika ofisi za BRELA jijini Dar es Salaam.*





*Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi wakimsikiliza Mwenyekiti, ambaye pia ni Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, Bw. Godfrey Nyaisa (hayupo pichani) wakati wa kikao kilichofanyika Machi 12, 2024 katika ofisi za Taasisi jijini Dar es Salaam.*





---




*Afisa Mtendaji Mkuu Bw. Godfrey Nyaisa akisisitiza jambo wakati wa kikao cha Baraza la Wafanyakazi kilichofanyika tarehe 12 machi, 2024 katika Ofisi za BRELA, Dar es Salaam*



*Washiriki wa kikao kazi cha kuandaa utaratibu wa kutambua vihatarishi kwenye kampeni wakiwa katika picha ya pamoja na mgeni rasmi katika ukumbi wa hoteli ya Morena, Morogoro.*



*Wawakilishi na wadau mbalimbali kutoka Taasisi za Udhibiti wakifuatilia mada kuhusu dhana ya Umiliki Manufaa wakati wa kikao kazi kilichofanyika Morena Hotel, Morogoro.*



*Afisa Usajili kutoka Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali Zanzibar (BPRA) Bi Raifa Hafidh Yahya, akiwasilisha mada kwa maafisa na wadau kutoka Taasisi za Udhibiti wakati wa kikao kazi kilichofanyika katika ukumbi wa Morena Hotel, Morogoro.*







Watumishi wa BRELA Bw. Seleman Seleman na Bi. Walta Komba wakikabidhi vyeti vya usajili wa majina ya biashara wateja waliofika banda la BRELA kupata elimu na huduma wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Mzumbe na Kambi ya Ujasiriamali yaliyofanyika Machi, 2024 Mzumbe, Morogoro



Mkurugenzi wa Miliki Ubunifu kutoka BRELA, Bi. Loy Mhando (katikati) na Mkuu wa Wilaya ya Mvomero Mhe. Judith Nguli (kulia) pamoja na Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu Mzumbe (kushoto) baada ya kukabidhi tuzo ya Mshindi wa Banda Bora ambayo BRELA ilitunukiwa.







Mtumishi wa BRELA Bw. Joram Manyika akimkabidhi cheti mwimbaji wa nyimbo za injili Bi. Christina Shusho baada ya kukamilisha usajili wa Jina la Biashara Machi, 2024 katika Ofisi za Wakala jijini Dar es Salaam.

# Usajili wa Miliki Ubunifu huongeza thamani ya bidhaa, huduma au kutoa ulinzi kwa wamiliki

**Na Stanislaus Kigosi**

Katika makala zilizopita tuliweza kuona na kuelewa dhana ya Miliki Ubunifu na umuhimu wake katika kukuza biashara pamoja na kuiangalia kwa ufupi mifumo ya kisheria inayosimamia ulinzi wa Miliki Ubunifu kitaifa, kikanda na kimataifa. Tunaamini kuwa hadi sasa wasomaji wetu wamepata uelewa kuhusu dhana ya Miliki Ubunifu pamoja na mifumo inayosimamia ulinzi wa Miliki Ubunifu.

Miliki Ubunifu kama ilivyo kwa mali nyingine zinazoshikika, pindi inapokuwa imerasimishwa na kupata ulinzi wa kisheria, ndivyo ambavyo thamani yake inavyoongezeka. Hii ni kama ilivyo kwa nyumba inayokuwa imejengwa katika kipande cha ardhi ambacho hakijarasimishwa kwa kusajiliwa na kupata hatimiliki, hata ingekuwa imejengwa kwa gharama kubwa, thamani yake haiwezi kuwa sawa na nyumba ya kawaida iliyojengwa kwenye kipande cha ardhi kilichorasimishwa na kupata hatimiliki. Vivyo hivyo, hata mali ya Miliki Ubunifu ambayo haijasajiliwa, thamani yake ni ndogo hata kama imeundwa kwa ubunifu mkubwa na wenye kuvutia sana.

Kwa kawaida sheria zinazosimamia ulinzi wa mali za Miliki Ubunifu kama vile Hakimiliki au Miliki Ubunifu zinazohusu uzalishaji wa viwandani haziwalazimishi wamiliki kuzisajili ili zilindwe. Sheria zote zimetoa hiari kwa wamiliki kusajili ama kutokusajili. Lakini kutokusajili mali zote zitokanazo na Miliki Ubunifu inaweza kufanya wamiliki kupoteza haki zao ambazo zimo katika Miliki Ubunifu pindi inapotokea kuwepo kwa migogoro ya umiliki au inapotokea uharamia umefanyika katika mali za Miliki Ubunifu.

Pamoja na kwamba kusajili Miliki Ubunifu kunatoa ulinzi kwa wamiliki, pia huongeza thamani ya mali za Miliki Ubunifu. Hivyo kuwafanya wamiliki kuweza kuitumia mali hiyo na kuwazuwia wengine kutumia mali ya Miliki Ubunifu bila ya ridhaa ya mwenye nayo. Ridhaa hiyo inaweza kuwa ni kwa kuuziwa au kukodishiwa ili mtu mwingine aitumie kwa wakati fulani kwa malipo maalum kama ambavyo wanaweza kukubaliana.

Usajili wa Alama za Biashara na Huduma mathalan humpatia mmiliki wa biashara na huduma husika nafasi ya kuitofautisha biashara au huduma yake na zile zinazotolewa na washindani wake. Pamoja na hayo huwazuia washindani wake kuweza kuiga alama yake ya biashara na huduma kwa kuiweka katika bidhaa au huduma wanazozitoa katika soko.

Wafanyabiashara kwa kawaida hutumia nguvu na gharama kubwa sana kufikisha bidhaa na huduma zao kwenye masoko pia kujenga uaminifu kwa wateja wao. Mara zote hutumia alama zao za biashara kutangaza bidhaa na huduma wanazozalisha. Hivyo, inaweza kutokea mfanyabiashara mmoja akatumia nguvu na gharama kubwa kujijenga kwenye soko kwa kutumia alama yake ya biashara, lakini kama hiyo alama yake ya biashara hajaisajili, basi, anaweza kukuta mshindani wake wa kibiashara ama ameamua kuisajili alama hiyo na hivyo kumfanya yeye asiweze kuitumia tena hiyo alama ya biashara ambayo kwa kiasi kikubwa tayari imeaminika na wateja.

Sambamba na hilo, katika mazingira sawa na hayo anaweza kutokea mfanyabiashara mwingine au mshindani katika biashara akaamua kughushi au kuitumia alama hiyo ya biashara kwa kutoa bidhaa au huduma duni tofauti na zile ambazo zinatolewa na mmiliki halisi wa alama ya biashara. Kitakachotokea katika mazingira haya ni kuvunja uaminifu ambao mmiliki wa alama husika ya biashara aliupata kutoka kwa walaji wa bidhaa na huduma zake. Hali hii ikitokea husababisha kuua biashara ya yule ambaye ni mmiliki halisi wa alama hiyo ya biashara na hivyo siyo tu kuathiri biashara ya mtu mmoja bali pia kuathiri mfumo wa biashara na uchumi wa nchi.

Kwa kawaida sheria za Miliki Ubunifu huwatambua na kuwalinda wale ambao wamefanya usajili wa mali zao za

> “Usajili wa Alama za Biashara na Huduma humpatia mmiliki wa biashara na huduma husika nafasi ya kuitofautisha biashara au huduma yake na zile zinazotolewa na washindani

Miliki Ubunifu na kuwalinda dhidi ya wengine ambao hawajafanya usajili. Hivyo, katika mazingira ya ushindani wa biashara, wafanya biashara ni lazima kuwa makini kwa kuhakikisha kuwa wanazilinda alama zao za biashara kwa kuzisajili kwenye ofisi ya Msajili wa Alama za Biashara ambayo kwa Tanzania Bara ofisi ya msajili ni Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA). Hii ndiyo ofisi inayotoa ulinzi wa Alama za Biashara na Huduma kwa mujibu wa Sheria ya Bunge Na. 12 ya mwaka 1986.

Aidha, linapokuja suala la ulinzi wa uvumbuzi ambao hulindwa na Sheria ya Hataza, mvumbuzi yeyote kabla hajauweka hadharani uvumbuzi wake inampasa aanze na utaratibu wa kusajili ulinzi wa hataza yake ndipo aweke hadharani uvumbuzi huo. Ieleweke kwamba uvumbuzi ndiyo chachu ya maendeleo ya teknolojia ambayo hutumika katika uzalishaji wa bidhaa viwandani, kutoa huduma za afya kwa kuja na vifaa tiba pamoja na dawa za matibabu na chanjo za magonjwa mbalimbali.

Mvumbuzi anapoacha kusajili uvumbuzi wake kwenye Ofisi ya Msajili wa Hataza ambayo kwa hapa Tanzania ni BRELA, uvumbuzi wake unaweza kuibwa na watu wengine ambao wanaweza kuutumia uvumbuzi huo kujinufaisha wao wenyewe kiuchumi bila mvumbuzi kunufaika kwa lolote. Ifahamike pia kuwa uvumbuzi ukisajiliwa na kupata cheti cha Hataza unaweza kuuzwa kwa wazalishaji ambao wao wanaweza kuuzalisha kwa wingi au kuitumia teknolojia hiyo kuzalisha dawa na vifaa tiba na kumpa mbunifu binafsi faida za kiuchumi pia kuongeza tija na kipato kwa nchi yetu.

# Wajasiriamali SIDO wajengewa uwezo kuhusu Alama za Biashara na Huduma




*Afisa Usajili wa BRELA Bi. Moreen Kitunisa akimsaidia mdau kukamilisha usajili wa Jina la Biashara wakati wa mafunzo ya Wajasiriamali SIDO kujengewa uwezo kuhusu Alama za Biashara na Huduma.*

**Na Njwaba Mwaijibe**

BRELA imewajengea uwezo wajasirimali kutoka Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) kwa kuwapatia elimu ya Alama za Biashara na Huduma katika ofisi za SIDO jijini Dar es Salaam.

Akitoa mafunzo hayo, Afisa Usajili Msaidizi wa BRELA, Bw. Athumani Makuka, alisema, Alama ya Biashara na Huduma ndio kitu pekee kinachoweza kutofautisha bidhaa yako na mzalishaji mwingine ikiwa ni pamoja na kuhimili ushindani katika soko na kuendeleza umaarufu wa ubora wa bidhaa na huduma.

Mbali na hayo Bw. Makuka alisema kuwa usajili wa Alama ya Biashara na Huduma inatoa haki ya kipekee ambayo wengine hawawezi kuitumia bila ridhaa ya mmiliki.

Aliongeza kuwa hasara za kutumia Alama ya Biashara na Huduma ambayo haijasajiliwa ni kukosa ulinzi wa kisheria pamoja na kuibiwa alama ya biashara yako.

Naye Bi. Antonia Masoyi, mratibu wa mafunzo hayo kutoka, SIDO alishukuru BRELA kwa kuungana na SIDO kwa ajili ya kutoa elimu kwa wajasiriamali kuongeza chachu ya kuendelea kufanya shughuli zao katika mifumo rasmi na kuongeza ushindani.

Mshiriki wa mafunzo hayo, Bw. Samson Clementia, alihitimisha kwa kusema kuwa mafunzo hayo yamewasaidia kuelewa namna bora ya uendeshaji wa biashara kulingana na matakwa ya kisheri na kuweza kumudu soko la ushindani.

# Changamkieni fursa urasimishaji biashara, Chuo Kikuu Mzumbe wahimizwa

**Na Gloria Mbilimonywa**

BRELA imeitaka jumuiya ya Chuo Kikuu cha Mzumbe, Morogoro, kuchangamkia fursa ya kurasimisha biashara zao ili ziweze kutambulika na kulindwa kisheria.

Rai hiyo ilitolewa na Mkurugenzi wa Miliki Ubunifu wa BRELA, Bi. Loy Mhando, wakati akiwasilisha mada kwa niaba ya Afisa Mtendaji Mkuu kuhusu umuhimu wa kurasimisha biashara katika Maadhimisho ya Siku ya Mzumbe na Kambi ya Ujasiriamali 2024.

Maadhimisho hayo yalifanyika Chuo Kikuu cha Mzumbe, Kampasi Kuu Morogoro, kuanzia Machi 20 hadi 22, 2024.

"Zipo faida nyingi zitokanazo na kurasimisha biashara ikiwemo, urahisi wa kufikiwa kwa huduma mbalimbali kwa kuwa kutawezesha kupata takwimu sahihi za biashara, vilevile biashara hizo zitatambulika kisheria. Vilevile, mfanyabishara ataweza kuweka hesabu vizuri na kuweza kupata huduma mbambali ikiwemo ikiwemo mikopo," alisema Bi. Mhando.

Bi. Mhando aliongeza kuwa urasimishaji biashara utawezesha wafanyabiashara kulipa kodi ambayo itachangia katika kukuza uchumi wa taifa utakaowezesha ujenzi wa miundombinu ya kuwafikia wafanyabiashara sambamba na ujenzi wa masoko na uwekaji wa mazingira wezeshi ya biashara.




*Waliosimama ni wajumbe wa jopo la majaji, akiwemo Afisa Usajili wa BRELA, Bi. Walta Komba, (wa tatu kutoka kushoto) wakiwa katika picha ya pamoja na Mkuu wa Wilaya ya Mvomero, Judith Nguli, (aliyekaa katikati pamoja na Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu Mzumbe Prof. Mwegoha (aliyekaa kushoto) wakati wa kuhitimisha Maadhimisho ya Siku ya Mzumbe na Kambi ya Ujasiriamali*

Naye Bw. Iddi Mohamed, mwanachuo wa mwaka wa pili katika Chuo hicho, alieleza kuwa amefurahishwa na elimu iliyotolewa na BRELA na kwamba awali alikuwa na mawazo ya kuanzisha biashara yake lakini hakufahamu nini afanye, baada ya kupata elimu ya urasimishaji kutoka BRELA amepata uelewa kuwa ukisajili kampuni yako au kurasimisha biashara kwa ujumla, unapata ulinzi wa kisheria na ikitokea changamoto yoyote inakuwa rahisi kukabiliana nayo.

Katika Maadhimosho ya Siku ya Mzumbe na Kambi ya Ujasiriamali 2024, BRELA ilishiriki kwa kutoa mafunzo maalum juu ya namna ya kurasimisha biashara na kulinda bunifu wanazozifanya sambamba na kutoa huduma ya usajili wa papo kwa papo kwa wanafunzi, wahadhiri na wafanyabiashara waliotembelea katika Maadhimisho hayo. Pia BRELA iliibuka mshindi wa Banda Bora na kukabidhiwa tuzo ya ushindi huo.

Maadhimisho hayo yaliyobeba Kauli Mbiu isemayo "Kuzingatia Teknolojia Zinazoibukia na Njia Mpya za Kujifunza kwa ajili ya Ukuaji Endelevu", yanatarajiwa kuhitimishwa tarehe 22 Machi, 2024. Kauli Mbiu hiyo inayolenga kuibua vipaji na mawazo bunifu ya wanafunzi wa Chuo hicho na pia kutoa nafasi kwa wafanyakazi na wanafunzi kuonesha ubunifu walionao.

# Wamiliki manufaa kufikiwa Dodoma

**Na Sheila Mfunami**

BRELA imewahimiza wamiliki wa kampuni kuwasilisha taarifa za wamiliki manufaa pamoja na taarifa za mwaka.

Wito huo umetolewa Machi 27, 2024, na Afisa Sheria Mkuu wa BRELA, Bw. Harvey Kombe, wakati wa ukaguzi elimishi kwa wafanyabiashara waliokuwa wakipata elimu kuhusu dhana ya wamiliki manufaa.

Akizungumza na wafanyabiashara hao, Bw. Kombe alisema zoezi hilo limelenga katika kutoa elimu juu ya dhana ya wamiliki manufaa na kuhimiza wafanyabiashara kuwasilisha taarifa za wamiliki manufaa sambamba na taarifa za mwaka za Kampuni.



*Mtumishi wa BRELA Bi. Everyn Mwamafupa akitoa elimu kwa mfanyabiashara wakati wa zoezi la ukaguzi elimishi Machi, 2024 jijini Dodoma.*

“Lengo kuu ni kuwapa elimu wafanyabiashara ambao bado hawajawasilisha taarifa zao za mwaka (*Annual returns*) na taarifa za wamiliki manufaa (Beneficial Ownership) na wale ambao tayari wamewasilisha ili kutekeleza matakwa ya kisheria baada ya usajili”, alisema Bw. Kombe.

Pia alitumia fursa hiyo kuwasikiliza na kupokea changamoto wanazokumbana nazo wakati wa kupata huduma za BRELA kupitia mfumo wa usajili kwa njia mtandao. Ukaguzi huu elimishi kuhusu Wamiliki Manufaa uliendelea kufanyika katika Jiji la Dodoma hadi Machi 28, 2024.




*Afisa Sheria Mkuu wa BRELA Bw. Harvey Kombe akizungumza na baadhi ya wafanyabiashara wakati wa zoezi la ukaguzi elimishi lililofanyika Machi, 2024 jijini Dodoma.*

## JIHUDUMIE POPOTE ULIPO

# PAKUA FOMU UNAYOTAKA TOKA KATIKA TOVUTI YETU

**www.brela.go.tz**

**Fomu**

- Fomu za Makampuni
- Fomu za Majina ya Biashara
- Fomu za Alama za Biashara
- Fomu za Hataza



BRELA
BUSINESS REGISTRATIONS AND LICENSING AGENCY

**Kwa maelezo zaidi:**
+255 22 2212800
ceo@brela.go.tz
usajili@brela.go.tz

BRELA
BUSINESS REGISTRATIONS AND LICENSING AGENCY

# A CALL FOR COMPANIES TO FILE ANNUAL RETURNS

The Registrar of Companies invites companies incorporated in Tanzania to file annual returns as required by the Companies Act, Cap 212.

**HOW TO FILE ANNUAL RETURNS THROUGH THE ONLINE REGISTRATION SYSTEM**

1.Log in on the Online Registration System (ORS)
2. Select e-service
3. Select company
4. Select Filling of annual return (accounts)/update
5. Fill in Compliance number
6. Fill in Company's details
7. Upload form 128 with signed and dated consolidated form and the latest Audited Accounts
8. Select mode of payment (Mobile or Bank)
9. After payment the application will be received for review.

**Note:** Filing fee of an annual returns is TZS 22,000 if submitted on time. Delayed submission of an annual returns attracts a late filing fee of TZS 2,500 (compounded) per every month delayed or part thereo




BRELA House, Plot No.. 23
Sokoine Drive / Shaaban Robert
P.O. Box 9393, 11101, Dar es Salaam,
Tel: +255 22 2212800
E-mail: ceo@brela.go.tz • usajili@brela.go.tz
Web: www.brela.go.tz

BRELA
BUSINESS REGISTRATIONS AND LICENSING AGENCY

# INVITATION FOR FOREIGN COMPANIES TO FILE FINANCIAL STATEMENT



The Registrar of Companies call all foreign companies with registered branches in Tanzania to submit their Financial Statement as required by the Companies Act, Cap 212.

## HOW TO FILE FINANCIAL STATEMENTS THROUGH THE ONLINE REGISTRATION SYSTEM

1.Log in on the Online Registration System (ORS)
2. Select e-service
3. Select company
4. Select Filling of annual return (accounts)/update
5. Fill in Compliance number
6. Fill in Company's details
7. Upload audited financial statement together with consolidated form
8. Click proceed button
9. An application will be received by Business Registration and Licensing Agency (BRELA) for review and process
10. After the review and processing of an application, an invoice will be sent to the customer for the payment of the required fee.

**Note:** Submission of financial statement costs USD 220.00 if submitted on time. Delayed submissions of financial statement are charged USD 25.00 (compounded) per every delayed month.




Jengo la BRELA, Kitalu Na. 20, Kiwanja Na. 23
Sokoine Drive / Mtaa wa Shaaban Robert
S.L.P 9393, 11101, Dar es Salaam, simu: +255 22 2212800
Barua Pepe: ceo@brela.go.tz • usajili@brela.go.tz
Tovuti: www.brela.go.tz

brela_tanzania | BRELA Tanzania | brela_tanzania | +255 (0) 735 331 003 | BRELA ONLINE TV